




**Wimbi** la talaka kwa wanandoa lazidi kutikisa

UKURASA 3




UKURASA 9

**Nipashe**

Jumatano Aprili 26, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581292

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



# Mchakato Katiba Mpya sasa rasmi

• **Waziri** Ndumbaro asema ni kupaumbele kwa mwaka 2023/24... *Endelea ukurasa wa 2*

## FCC yatakiwa kutekeleza uamuzi wa mahakama uuzaji Tanga Cement

UKURASA 3



Baadhi ya wakazi wa Malulu, Tarafa ya King'ori, jijini Arusha na askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wakitumia 'kijiko' kulivuta gari aina ya Toyota Noah, lililokuwa na wanafamilia watano baada ya kusombwa na maji jana na kusababisha vifo vya watu watatu na wawili kujeruhiwa. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Mvua yaua watatu wa familia moja, yakata barabara ya Moshi hadi Arusha

UKURASA 2



## Rais Samia, Mwinyi wanavyotembea katika sura halisi ya Muungano

UKURASA 10

**MICHEZO** SIMBA SC KIMBINU ZAIDI MOROCCO UK.24 **KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mchakato Katiba mpya sasa rasmi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MCHAKATO wa kupata Katiba mpya sasa ni rasmi baada ya Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, jana kulieleza Bunge kwamba ni moja ya vipaumbele vitakavyotekelezwa na wizara yake kwa mwaka 2023/24.

Mchakato huo ulikwama Aprili 2, 2015 kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kutangaza kuahirisha kura ya maoni ya Katiba Inayopendekezwa iliyokuwa ifanyike Aprili 30, mwaka huo, hadi itakapotangazwa tena.

NEC ilitoa sababu za kuahirishwa huko kuwa ni kutokukamilika kwa uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa njia ya kielektroniki (BVR).

Jana, akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2023/24, Waziri Ndumbaro aliomba kuidhinishiwa Sh. bilioni 383.6, Dk. Ndumbaro huku akisema kati ya vipaumbele 30 watakavyovitekeleza kwa mwaka ujao ni mchakato wa Katiba mpya.

Alisema mbali na kuratibu mchakato huo, pia watatekeleza mkakati wa kutoa elimu ya Katiba kwa umma pamoja na kufanya marekebisho ya sheria za uchaguzi na demokrasia.

Dk. Ndumbaro alitaja kipaumbele kingine ni kutekeleza kampeni ya Mama Samia Legal Aid kwa Watanzania.

Alitaja vipaumbele vingeni ni kuwasilisha taarifa kwenye vikao na majukwaa ya haki za binadamu na watu katika ngazi ya kikanda na kimataifa, kutekeleza programu ya kutumia lugha ya kiswahili katika utoaji haki nchini.

"Kipaumbele kingine ni kuwasilisha taarifa tatu za nchi kuhusu utekelezaji wa mikataba mitatu ya haki za binadamu ambayo serikali imeridhia," alisema Dk. Ndumbaro.

Vipaumbele vingine ni kuendelea kutafsiri sheria za nchi kutoka lugha ya kingereza kuwa katika lugha ya kiswahili, kuendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki ili haki ipatikane kwa wote na kwa wakati.

Vingine ni kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala kwa kuanzisha na kuendesha Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro, kuimarisha mfumo wa elimu ya sheria, kuratibu mapitio na marekebisho ya sheria za sekta ya sheria.

Dk. Ndumbaro alivitaja pia vipaumbele vingine ni kuandaa sera mahususi zinazosimamia mifumo ya utoaji haki, kuendelea kuimarisha mfumo wa uangalizi wa utajiriasili na maliasilia za nchi.

Vingine ni kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma za sheria, kuendelea na ujenzi wa vituo jumuishi vya taasisi za sheria, kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya kikatiba na utawala wa sheria.

Pia alisema wizara itaendelea kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro ambazo ni usuluhishi, upatanishi, maridhiano na majadiliano ili kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa haki nchini.

Sambamba na hivyo, alisema vipaumbele vingine ni kuimarisha mifumo ya kuhamasisha, kuzingatia na kulinda haki za binadamu, kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Taifa wa Haki Mtoto 2020/21-2024/25.

Alitaja kipaumbele kingine ni kuendelea kuimarisha usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu pamoja na shughuli za ufilisi na udhamini.

"Pia tutaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya tume na kamati za maadili ya maofisa wa Mahakama ngazi ya mikoa na wilaya, kufanya tafsiri, uandishi na urekebu wa sheria, kutoa ushauri wa kisheria na kufanya upekuzi na marejeo ya mikataba," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisema pia wizara itaendelea kuimarisha uendeshaji mashtaka na usimamizi wa kesi za jinai, kuimarisha uratibu na usimamizi wa upelelezi wa makosa ya jinai na kuimarisha mfumo wa utaifishaji mali, usimamizi na urejeshwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu, kuimarisha utekelezaji wa programu ya kutenganisha shughuli za mashtaka na upelelezi.

Alitaja kipaumbele kingine ni kuratibu, kusimamia na kuiwakilisha serikali na taasisi zake katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya serikali katika Mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi na kufanya uchunguzi kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.



## Watu 10 waugua kipindupindu Dar

**Na Jenifer Gilla**

WIZARA ya Afya imetangaza kuwapo kwa mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu katika wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam huku ikibainisha kuwa watu 10 wamethibitika kuugua tangu kuripotiwa Aprili 20, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na wizara juzi, ilisema mara ya kwanza ugonjwa huo uliripotiwa eneo la Kivule na kwamba watoto wawili wa familia moja, mmoja akiwa mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kivule, walithibitika kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, watu wanne, wawili wanawake na wawili wanaume kutoka familia moja walithibitika kuwa na dalili za ugonjwa huo na sasa wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kivule .

"Dalili za ugonjwa huo zilianza kuonekana kuanzia Aprili 19, 2023. Visa vyote vinne vya ugonjwa huo wa mlipuko vimetokea kwa wanafamilia wanaoishi kaya moja kata ya Kivule, Mtaa wa 10.

Aidha taarifa hiyo ilisema visa vitatu vipya viliripotiwa katika maeneo ya Tabata, Ilala na Buguruni na kuwa katika kesi zote 10 zilizoropotiwa hakuna vifo vilivyorekodiwa.

"Tunaendelea kufanya utafiti ili kutambua visa vingine, tunakusanya sampuli za maji kwenye visima na maji ya bomba, pamoja na vyanzo vingine vya maji kwa ajili ya majaribio," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Katika kudhibiti kuenea kwa kasi kwa ugonjwa huo wizara imeanzisha Kituo cha Matibabu ya Kipindupindu katika Hospitali ya Wilaya ya Kivule.

# Mvua yaua watatu wa familia moja

**Na Waandishi Wetu**

WATU watatu wa familia moja wamepoteza maisha na wengine wawili kuokolewa baada ya gari aina ya Toyota Noah walilokuwa wakisafiria kusombwa na maji.

Tukio hilo lilitokea jana asubuhi eneo la Konoike Malula, wilayani Arumeru mkoani Arusha.

Gari hiyo ilikuwa imebeba abiria watano ambao watatu kati yao, wamepoteza maisha na wengine wawili akiwamo dereva, waliokolewa na wanaendelea na matibabu.

Kutokana na tukio hilo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Emmanuela Kaganda, amewataka wananchi kuchukua tahadhari na kuwa makini ikiwamo kutodharau maji hasa kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha.

Akizungumza na wananchi wa eneo hilo ilikotokea ajali hiyo, kiongozi huyo alisema wamepokea kwa huzuni tukio hilo na kutoa pole kwa familia zilizopoteza wapendwa wao.

Mkuu wa wilaya hiyo, aliwakumbusha wananchi kuenzi utamaduni za Kitanzania pale ambapo tatizo linapotokea badala ya kujikita kupiga picha. Pia aliwahimiza watembea kwa miguu na wanaotumia vyombo vya moto kutokuingia kwenye maji yanayopita kwenye barabara au maeneo mengine bila kuchukua tahadhari.

Alisema dereva wa gari lililosombwa na maji, Naiman Metili, alijaribu kuvuka bila kujua nguvu ya maji hayo.

Wakati huo huo, abiria waliokuwa wakisafiri jana asubuhi kwa kutumia barabara kuu ya Moshi-Arusha, walijikuta wakikwama kwa saa tatu mfululizo eneo la Kwa Msomali baada ya Mto Biriri kufurika maji.

Kutokana na hali hiyo, watumiaji wa barabara hiyo yakiwamo mabasi yanayokwenda mikoa mbalimbali nchini, abiria wake walikwama eneo hilo huku wakilalamika kuchelewa safari zao.

Tukio la aina hii lilitokea wiki mbili zilizopita eneo hilo na kuleta usumbufu kama huo kwa watumiaji wa barabara hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, mmoja wa abiria hao, mfanyabiashara wa mitumba katika soko la Memorial, Anna Celestine, alisema serikali inatakiwa kutatua tatizo hilo ili kutokwamisha maendeleo.

"Wafanyabiashara tunatoka Arusha kuja sokoni, tunacheleweshwa na maji. Hili si jambo la mara ya kwanza, serikali inajua na Mbunge anajua ila hakuna wanachotusaidia zaidi na wao kunung'unika," alisema.

Naye Leonard Bantaleo alisema: "Hali hii itasababisha madereva kukimbiza magari ili kufika mapema kufidia muda wanaopoteza hapo. Serikali iongezi usimamizi na kufanya ukarabati wa miundombinu yake kwa wakati," alisema.

Akiwa katika eneo hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, pamoja na kamati yake ya ulinzi na usalama, alisema mvua iliyonyesha katika maeneo ya milimani imesababisha mafuriko na baadhi ya magari kushindwa kupita.

"Kutoka alifajiri magari yote yaliyotokea Arusha kwenda Moshi kwa ajili kwenda mikoa mbalimbali ikiwamo Tanga, Pwani na Dar es Salaam hayajaweza kupita na yote yanayotoka Moshi kwenda Arusha kwa ajili ya kwenda mikoa Singida, Dodoma na Mwanza yameshindwa kupita katika daraja hili.

"Kwa sasa kwa kushirikiana na askari ameanza kuruhusu magari ya upande mmoja, tunatoa wito kwa madereva wa magari ya abiria na binafsi hasa kipindi hichi cha masika wachukue tahadhari wasije wakasababisha ajali," alisema.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Benito Msovela, alisema: "Tayari tulishawasiliana na mtendaji mkuu na tumepata kibali cha kujenga daraja kubwa katika eneo hili. Hutujaanza ujenzi kwa sababu kipindi hiki ni cha mvua zitakapokwisha tutajenga pamoja na kuinua barabara ili maji yasipite juu ya barabara." alisema.

**Imeandaliwa na Allan Isack, (ARUMERU) na Mary Mosha (HAI).**

## HABARI KITAIFA



Madaktari Bingwa wa upasuaji wa watoto wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), wakishirikiana na wataalam kutoka nchini Marekani na Italia, wakimfanyia upasuaji wa kunyoosha mgongo uliopinda (kibiongo) mgonjwa jijini Dar es Salaam jana, ambapo wagonjwa zaidi ya sita wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji huo. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Kasi ya talaka yazidi kutikisa

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

TAKWIMU za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, mwaka huu, zinaonyesha kuwa talaka 410 zilisajiliwa kulinganisha na kipindi kama hicho Julai 2021 hadi Machi, 2022 zilizokuwa 303.

Takwimu hizo zinaonyesha kuongezeka kwa utolewaji kwa idadi ya 107.

Pia kwa kipindi cha Julai, mwaka jana, hadi Machi, mwaka huu, wakala ulipokea marejesho 31,376 ya ndoa zilizofungwa kulinganisha na kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 iliposajili ndoa 26,303.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alibainisha hayo jana bungeni jijini hapa wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa wizara yake kwa mwaka 2023/24.

"Wizara kupitia RITA inaendelea na usajili wa matukio ya ndoa na talaka. katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, umepokea marejesho 31,379 ya ndoa zilizofungwa na nakala za hukumu za talaka 410 na kusajiliwa," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema Wizara ya Katiba na Sheria kupitia RITA imeendelea na jukumu ya usimamizi na usajili wa bodi za wadhamini, kwamba katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 bodi za wadhamini 68 zilisajiliwa.

Dk. Ndumbaro alisema katika kuboresha utendaji wa bodi hizo, wakala iliandaa Katiba mfano ambayo inatakiwa kufuatwa na bodi zote za wadhamini zilizosajiliwa RITA na zinazotarajiwa kusajiliwa.

Kadhalika, alisema wizara kupitia RITA iliendelea na jukumu la kuhamasisha wananchi kuandika na kuhifadhi wosia ili kupunguza migogoro ya kugombea mali inayojitokeza katika jamii baada ya mzazi mmoja kufariki.

Alisema kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 wosia 97 zilitayarishwa na kuhifadhiwa.

Aidha, alisema RITA ilifanya utafiti kuhusu uwapo wa mwamko mdogo wa kuandika wosia katika jamii, lengo likiwa ni kubainisha sababu zinazofanya wananchi wengi kutoandika na kuhifadhi wosia.

Dk. Ndumbaro alisema utafiti huo ulifanyika kwa kuchagizwa na kaulimbiu ya "Familia Kwanza Andika Wosia Sasa", kwamba taarifa ya matokeo ya utafiti huo inatarajiwa kutolewa hivi karibuni na kutumika katika mipango na mikakati ya kuimarisha huduma za menejimenti ya uandishi na utunzaji wa wosia kwa umma wa Watanzania.

# FCC yatakiwa kutekeleza uamuzi mahakama kuhusu Tanga Cement

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Ushindani Tanzania (FCC), imetakiwa kutekeleza uamuzi wa kisheria uliotolewa kuhusu mchakato wa uuzwaji kwa Kampuni ya Saruji Tanga kwa Kampuni ya Saruji ya Twiga.

Imeelezwa kuwa kumekuwa na taarifa zinazokiuka uamuzi wa Baraza za Ushindani wa Biashara (FCC) kutaka mchakato usimame huku baadhi ya watu wakielezea kuwa kuna faida juu ya ununuzi wa hisa za Tanga Cement ambao unatarajiwa kufanywa na Twiga Cement.

Licha ya FCC kutakiwa kufanya hivyo, Rais Samia Suluhu Hassan ameshauriwa kutokuingia kwenye mtego utakaosababisha kupanda kwa bei ya saruji ikiwa Twiga itachukua Tanga Cement.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Heche , alisema hayo jana jijini Mwanza wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Heche alisema sheria za nchi katika eneo la ushindani na haki za mradi ziko wazi katika kupusha mfumo wa udhibiti wa soko la saruji kwa lengo la kuwalinda watumiaji wa bidhaa au huduma husika. Alisema kitendo cha FCC kushindwa kufuata sheria na hukumu ya mahakama juu ya uuzwaji wa Tanga Cement, ni hatua ya kutaka kuwakandamiza wananchi ambao ni watumiaji wakubwa wa saruji.

Heche alisema mpaka sasa serikali imeshindwa kutekeleza hukumu iliyotolewa juu ya kuzuia Twiga Cement kutouzwa.

'Kwa nini mtu mmoja aumize wananchi kwa maslahi yake au kikundi fulani? Mchakato wa kuifanya Twiga Cement kuinunua Tanga Cement utafanya bei ya saruji kupanda na kusababisha wananchi washindwe kujenga. Kuna chama cha walaji (watumiaji) kilienda mahakamani kufungua shauri kwa sababu sheria yetu inakataza kesi namba 6/2022 wakashinda na kuagizwa kwamba serikali izuie Twinga Cement kununua Tanga Cement," alisema.

Pia alisema alisema yeyey na wenzake kama viongozi wa kisiasa, wana wajibu na jukumu kuwasemea wananchi, hivyo suala hilo ni hatari na litasababisha wananchi kuingia katika matatizo makubwa ya kununua saruji kwa gharama ya juu. Pia alisema hali hiyo itsababisha watu wenye matumaini ya kujenga na kutoka katika nyumba za kupanga kushindwa kumudu gharama hizo.

Alisema nchini Tanzania bei ya saruji ni kubwa kuliko nchi yoyote ya Afrika Mashariki na Kati kwa kuwa mfuko wa saruji mmoja kwa Kenya ni Sh. 9,000 huku Tanzania ikifikia Sh. 15,000 hadi 17,000 kwa Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Heche, ni vyema FCC na serikali zikafuate amri ya Baraza la Ushindani (FCT) ya kuzuia mchakato wowote wa kuuza kwa Tanga Cement kwenda Twinga Cement na kuhakikisha uamuzi huo unaheshimiwe kwa kuwa kuendelea na mchakato ni kudharau amro halali ya baraza ambalo liko kisheria.

"Tume ya Ushindani inapaswa itekeleze wajibu wake kama ilivyoanzishwa ikiwamo kusimamia ushindani wa haki na kuhakikisha mradi wa bidhaa na si kugeuka kuwa waathirika wa wafanyabiashra. Pia Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara naye anapaswa kujitafakari juu ya hili kwani ni kipimo cha serikali katika kufuata sheria na utaratibu tuliojiwekea kama nchi," alisisitiza.


IGALULA AUCTION MART LIMITED

Dealers in: General Auctioneers Collection service, Real estate Agent, Valuers and Commission Agent.

Head Office
Masdo House
Samora /Azikiwe Street
Email igalulaauctionmartltd@gmil.com
Tell: +255 (0) 652-014363

Yard Office
Mbezi Beach
Bagamoyo Roads
P.o Box 45189
Dar es Salaam
Tell: +255 (0) 689-690292

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**IGALULA AUCTION MART LIMITED** kwa idhini waliyopewa na **BANK OF INDIA (TANZANIA) LIMITED,** S. L. P. 7581, DAR ES SALAAM. kwa mujibu wa hati ya rehani iliyosainiwa na wahusika, tutauza kwa mnada amana ilizoainishwa hapa chini kama ifuatavyo: -

| Jina la Mdaiwa | Jina la Mwenye Mali | Maelezo ya Mali | Tarehe na Muda |
|---|---|---|---|
| AK'S Limited, Mtaa wa Zanaki/Indira Gandhi, S. L. P. 1450, Dar es Salaam, Tanzania | Mukesh Vrajlal Kanabar, S. L. P. 2915, Dar es Salaam, Kiwanja Nambari 448, Eneo la Ujazo Mdogo, Kawe, Jiji la Dar es Salaam. | Nyumba, ardhi na maendeleo yote yaliyofanyika kwenye Kiwanja Nambari 448, Eneo la Ujazo Mdogo, Kawe, Jiji la Dar es Salaam [Hati Nambari 32530] | Tar. 12/05/2023, Saa nne asubuhi (*04:00*) |

**Masharti ya Mnada**

1. Mshindi atalipa asilimia 25% papo hapo baada ya nyundo ya dalali kushuka. Kiasi kinachobakia, yaani asilimia 75% kitalipwa ndani ya siku 14 (kumi na nne) baada ya siku ya mnada. Atakayeshindwa kulipa hiyo asilimia 75% katika muda huo, ushindi wake utafutwa na hatarudishiwa kiasi alichotanguliza. Mali hiyo itanadiwa tena.
2. Nyumba inauzwa katika hali iliyonayo (as is where is basis).
3. Siyo lazima mwenye kutoa bei ya juu ashinde. Benki ina haki ya kuweka kiwango cha chini ambacho lazima kifikiwe (reserved price).
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

217395701

KWA MAELEZO ZAIDI, UNAWEZA KUWASILIANA NA DALALI KUPITIA ANWANI ZILIZOPO HAPO JUU.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akibonyeza kitufe kuzindua Baraza la Kutokomeza Malaria wakati wa maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam jana. Kulia ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na katikati ni Mwenyekiti wa Baraza hilo, Leodegar Tenga. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Malaria bado tishio, mamilioni ya Watanzania hatarini kuugua

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema asilimia 94 ya Watanzania wako katika hatari ya kupata ugonjwa wa malaria kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya zaidi ya asilimia 70 ya mbu kujenga usugu dhidi ya dawa aina ya pareto.

Amesema dawa hiyo ni ile ambayo huwekwa kwenye vyandarua vinavyotumika kwa muda mrefu nchini.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani na kusema, licha ya serikali kupunguza maambukizi mapya kutoka asilimia 14.8 mwaka 2015 hadi asilimia 8, mwaka huu, lakini bado ugonjwa huo upo na unaleta madhara ikiwamo vifo.

"Watu kushindwa kufanya shughuli za maendeleo pale wanapougua, hawaendi shambani, hawaendi viwandani, hawafanyi uzalishaji na watoto wetu wanaweza kupoteza siku tano hadi saba za kuwapo shuleni, kwa hiyo malaria bado tishio katika nchi yetu," alisisitiza.

Waziri alisema wizara kwa kushirikiana na wadau wanatekeleza mpango Mkakati wa Taifa wa Miaka Mitano wa Kutokomeza Malaria uliojikita kwenye maeneo manne ikiwamo udhibiti wa mbu waenezao malaria, uchunguzi, kinga na tiba, ufuatiliaji na tathmini ya ugonjwa.

Aidha alisema wamefanikiwa kupunguza mikoa yenye kiwango kikubwa cha malaria chini ya asilimia moja kutoka sita, mwaka 2017 hadi mikoa tisa, mwaka huu ikiwamo Dar es Salaam na Kilimanjaro.

Alisema lengo kwa baadhi ya mikoa ni kufikia asilimia sifuri ya maambukizi ifikiapo mwaka 2025.

Aidha, alisema wanaendelea kutoa elimu, kununua na kusambaza vitendanishi na dawa malaria katika vituo vya afya pamoja na kufuatilia ubora, usalama ufanishi wa dawa za malaria na wamejiridhisha kuwa asilimia 96 ya dawa hizo zinauwezo wa kutibu ugonjwa huo.

Katika maadhimisho hayo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitoa maagizo sita ikiwamo kwa wizara hiyo kuendelea kutumia taasisi za utafiti ili kujiridhisha na ubora wa vyandarua vya kisasa vyenye tija katika kukabiliana na maambukizi ya Malaria.

Ameiagiza wizara hiyo, kufanya kampeni ya kutosha ya kuhamashisha matumizi ya vyandarua vya kisasa hadi katika maeneo ya vijijini na kuzihimiza mamlaka za serikali, kuhakikisha vyandarua hivyo, vinatumika kwa lengo lililokusudia na tofauti na wengi kuvitumia mashamba ya mboga.

Vilevile, ameiagiza wizara pamoja na wadau kuhakikisha kuwa afua za mapambano dhidi ya ugonjwa huo zinaanza kutelezwa kwenye maeneo yanye kiwango cha maambukizi ya juu ili kuhakikisha ufikiwaji wa malengo ya kutekeleza ugonjwa huo nchini.

Pia, amewasihi Watanzania kuzingatia matumizi sahihi ya dawa za kutibu ugonjwa huo pamoja na maelekezo ya madaktari kuhusu tiba ikiwamo kutotumia dawa hizo bila kupima kwa kuwa, si kila ugonjwa ni malaria.

Majaliwa amewaagiza wajumbe wa Baraza la Kutokomeza Malaria alilolizindua wahamasishe upatikanaji wa rasilimali katika sekta zao ili kuchangia juhudi za serikali katika kutokomeza ugonjwa huo.

Baraza hilo lenye wajumbe 19 wakiwamo viongozi wa dini, mawaziri, manaibu na makatibu wakuu wa Wizara mbalimbali linaongozwa na Leodegar Tenga ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI).

"Baraza limesheheni watu makini sana, wabunifu na wenye weledi kwa hiyo wekeni mipango yenu vizuri kuhamasisha mapambano dhidi ya Malaria kuhakikisha mwaka 2030 tunatokomeza kabisa ugonjwa huu," alisema.

Aliwataka watumie ubunifu wao kuhamasisha wananchi kuacha kawaida ya kutumia dawa za Malaria bila kupata vipimo na wasisitize matumizi ya vyandarua vyenye dawa kwenye kaya zote.

Aliwaomba wadau mbalimbali kuendelea kushirikiana na serikali kukusanya rasilimali zitakazowezesha mapambano dhidi ya ugonjwa huo kufanikiwa.

"Licha ya takwimu kuonyesha kwamba maambukizi ya ugonjwa huu yanapungua lakini bado kuna maambukizi na watu wetu wanakufa hivyo kupunguza rasilimali watu na kuleta athari kwenye uchumi kwa hiyo lazima tuweke mikakati ya kutusaidia kuondokana na tatizo hili," alisema.

Alisema ili kuhakikisha ugonjwa huo unatokomezwa, Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza dawa za kutibu ugonjwa huo pamoja na vipimo vya MRDT viendelee kutolewa bure zikiwemo sindano.

Aliipongeza mikoa iliyofanikiwa kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo ukiwemo Mkoa wa Dar es Salaam lakini aliwataka wasibweteke na badala yake waendelee kuweka mipango ya kudhibiti ugonjwa huo.

Waziri wa Habari, Sayansi na Teknolojia, Nape Nnauye, aliagiza kampuni za simu na vyombo vyote vya habari kuweka mipango ya kuelimisha umma kuhusu athari za ugonjwa huo na hatua za kujikinga.

"Kampuni za simu na kampuni zingine zipo kwasababu watu wana afya kwa hiyo lazima wawe na mipango mikakati ya kutokomeza ugonjwa huu kwasababu Tanzania Bila Malaria inawezekana," alisema Nape.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limetenga Aprili 25 kila mwaka kuadhimisha siku ya Malaria duniani ili kuangazia juhudi za dunia za kutokomeza ugonjwa huo. Kwa mujibu wa shirika hilo, watu bilioni 3.3 duniani wako katika hatari ya kuugua huku mwaka 2012 ulisababisha vifo kwa watu takribani 627,000.

**•Imeandaliwa na Jenifer Gilla na Joseph Mwendapole**

## IMF yatoa bilioni 354/- kusaidia bajeti

**Na Mwandishi Wetu**

BODI YA Wakurugenzi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), imeipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wa Sh. bilioni 354, ikiwa ni sehemu ya mkopo wa Sh.trilioni 2.4 wa miaka mitatu kwa ajili ya kuchangia bajeti ya serikali ya mwaka 2022/23.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Arusha kuhusu mkopo huo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Fedha na Mipango, Benny Mwaipaja, alisema IMF imeridhishwa na sera nzuri na diplomasia ya uchumi inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan wakati ambao nchi mbalimbali duniani zinakabiliana na changamoto za kiuchumi.

Mwaipaja alisema fedha hizo ni sehemu ya makubaliano yaliyofikiwa mwaka jana ya kutoa Sh.trilioni 2.4 kwa awamu saba kuanzia mwaka 2022 hadi 2025.

"Sasa hivi ukienda nje ya nchi wawekezaji wengi wanataka kuja Tanzania, wanasema wanaridhishwa na hatua zilizochukuliwa. Hivi karibuni tulikuwa Marekani, wawekezaji wengi walikuwa wakiongea na waziri, unaona ile hamu ya kuja nchini kutokana na mabadiliko makubwa yaliyofanywa na Rais Samia," alisema.

Pia alisema Tanzania imekuwa nchi ya mfano duniani kwa kutumia vizuri fedha za mkopo wa masharti nafuu za UVIKO -19 ambazo zilielekezwa kwenye sekta za afya, miundombinu na elimu kwa kugusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

"IMF ilisema kabisa imeridhishwa na matumizi ya fedha hizi tofauti na nchi zingine walioshia kununua barakoa. Kwetu Rais Samia alizielekeza kwenye maeneo muhimu yanayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja. Tumesifiwa sana na kujenga imani kubwa kwao," alisema.

Mwaipaja alisema kabla ya fedha nyingine kutolewa, IMF hufanya tathmini na wanaporidhishwa, huridhia fedha zingine kutolewa na kwamba walifika nchini wakaona utekelezaji ndipo wakakubali mkopo huo kutolewa kwa awamu ya pili.

"Tunawashukuru IMF kwa mkopo huu ambao utakwenda kuleta mabadiliko kwa wananchi,tutaendelea na jitihada zote za kuboresha sera za kiuchumi ili kuvutia wawekezaji zaidi. Tunapewa hizi fedha kila mwaka mara mbili na ikifika 2025 tutapewa zote kwa pamoja.

"Utekelezaji wa mradi umekuwa wa viwango vya juu na kila vigezo vilivyowekwa na malengo yaliyowekwa vimefikiwa kwa wakati," alisema Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa IMF, Antoinette Sayeh, katika taarifa yake kwa umma.

## Kampuni yazipa vifaa vya mamilioni shule za serikali

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwassa ameipongeza Kampuni ya Alliance One Tobacco Tanzania Limited (AOTTL) kwa kutoa vifaa vyenye thamani ya Sh. 222,762,898 kwa shule mbili za msingi za Morogoro ambazo ni Kingolwira na Bungo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Fatma alisema anajivunia ukarimu wa kampuni na kuzitaka kampuni zingine kuiga mfano huo katika kusaidia jamii kwa kushirikiana na serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Sote tunajua kuwa kampuni inanunua tumbaku nchi nzima na zaidi Mkoa wa Tabora, lakini sisi wana Morogoro pengine tuna bahati kuliko wengine kwa sababu msaada ambao tumepokea leo ni mkubwa kuliko ile ya Tabora na mikoa mingine inayolima tumbaku," alisema.

Fatma aliahidi kwa niaba ya shule kutunza vyema vifaa vyote vilivyotolewa kwa kuhakikisha vinabaki katika hali nzuri kwa vizazi vijavyo.

Aliwapongeza walimu na wanafunzi kwa pamoja kutoka shule zote mbili zilizopokea mafunzo kwa kufanya vyema katika taaluma zao, ingawa idadi ya wanafunzi ilizidi idadi ya walimu dhidi ya kiwango kinachohitajika.

Alisema msaada huo utasaidia kuboresha mazingira ya ujifunzaji kwa wanafunzi.

Alisema Shule ya Msingi Bungo ina jumla ya wanafunzi 1,600 na Kingolwira ina wanafunzi takribani 2,000, lakini wote wanafanya vyema kitaaluma licha ya shule hizo kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, Ephraim Mapoore, Mkurugenzi wa Fedha wa AOTL, Festo Mwalongo alisema kampuni yake itaendelea kutoa msaada kwa Morogoro na maeneo mengine yanayolima tumbaku kwa kuzingatia sera zake za uwajibikaji wa kijamii na usimamizi wa mazingira kwa jamii.

"Alliance One itaendelea kutoa huduma kwa jamii kwa muda wote, tunatenga Sh. milioni 400 kila mwaka kwa ajili ya kazi hii nzuri ya kurudisha kwa jamii inayozunguka maeneo yetu ya kazi," alisema na kutoa wito kwa walimu na wanafunzi kuvitunza vifaa hivyo kwa kuwa vimetolewa kwa manufaa yao na kwa wale watakaojiunga na shule siku zijazo.

Akitoa maelezo ya michango hiyo katika hafla ya kukabidhi msaada huo iliyofanyika katika Shule ya Msingi Kingolwira, Msemaji Mkuu wa kampuni hiyo Wakili John Magoti alisema kampuni hiyo imejenga vyoo vya wanafunzi wenye ulemavu katika Shule ya Msingi Bungo vyenye thamani ya Sh. milioni 10.4 na kwa Shule ya Msingi Kingolwira alitaja vifaa vilivyotolewa kuwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa ya chekechea kwa gharama ya Sh. milioni 21.2 na pia kukarabati vyumba vitano vya madarasa kwa gharama ya Sh. milioni 48.3.

Alisema vifaa vingine vilivyotolewa kwa Shule ya Msingi Kingolwira ni pamoja na ujenzi wa jiko la shule lililokamilika na vifaa muhimu kwa gharama ya Sh. milioni 45.7 pamoja na kununua na kuunganisha umeme wa jua wenye thamani ya Sh. milioni 13.7 kwenye kisima chenye urefu wa mita 162 ambacho awali kilichimbwa na kampuni hiyo.

"Kampuni pia imejenga vyoo kwa ajili ya walimu, wanafunzi pamoja na vyumba mahususi kwa ajili ya wasichana vyenye thamani ya Sh. milioni 48.3," alisema na kuongeza kuwa kampuni hiyo pia imetoa mtambo mkubwa wa kusafisha maji wenye thamani ya Sh. milioni 35.3.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kingolwira, John Fulana alisema kwa sasa wanafunzi hao watakuwa hawakai tena sakafuni kama ilivyokuwa zamani.

"Pia tuna matumaini kuwa magonjwa yatokanayo na maji ambayo yalikuwa yameenea miongoni mwa wanafunzi wetu hapa sasa yatakuwa historia," alisema, akiongeza kuwa nishati ya jua itapunguza kwa kiwango kikubwa bili za umeme shuleni.

## Baba adaiwa kuwaua wanawe kwa sumu kisa hafanani nao

**Na Halfani Chusi**

SIKUKUU ya Eid Pili, haikuwa njema kwa wakazi wa Chanika Mwisho jijini Dar es Salaam, baada ya baba mzazi wa watoto watatu, Kareem Chamwande, kudaiwa kuwaua watoto wake wawili kwa sumu kwenye juisi akidai hafanani nao.

Tukio hilo lilitokea Jumapili usiku na sababu kubwa ikielezwa kuwa baba wa watoto hao alikuwa anamtuhumu mkewe kuwa mtoto mmoja ambaye ni mdogo wa mwisho si wake.

Baada ya tuhuma hizo zilizodumu kwa muda mrefu na kuzua ugomvi, mke aliamua kuepusha shari akaondoka na watoto wake kurudi nyumbani kwao.

Ilipofika Sikukuu ya Eid Pili, Chamwande alikwenda kuwachukua watoto ili awatoe kwa ajili ya kula sikukuu ndipo alipokwenda kuwapa juisi inayodaiwa kuwa na sumu ili awaue kisha naye ajiue.

Bahati mbaya, mmoja alifariki dunia kabla lengo lake la kujiua halijatimia, akambeba kumpeleka kwa bibi yao. Alipofika huko alimweka chini nje na kuanza kubomoa karo lengo likiwa halijafahamika mara moja kama alitaka kutumbukia humo au kumtumbukiza mtoto.

Raia wema kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walimkamata huku wale wengine wawili walikutwa wakiwa hoi na wakati wanapelekwa hospitalini, mmoja alifia njiani lakini mwingine bado anaendela na matibabu.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo huku akisema wako katika hatua ya kukamilisha uchunguzi ili kubaini chanzo cha mauaji hayo.

"Tunamshikilia Kareem Chamwande, ambaye anadaiwa kaua watoto wake wawili kwa kuwapa juisi yenye sumu na sasa tunashirikiana na mamlaka zetu za kisayansi kukamilisha uchunguzi huo kwa ajili ya kufikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa." alisema.

Maziko ya watoto hao wawili, Abrahaman Chamwande na Kauthar Chamwande, yalifanyika juzi usiku katika makaburi ya Kwa Mwarabu, Chanika.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Simu: 028-2227148
Nukushi: 028-2227140

Barua pepe: ded@karagwedc.go.tz
Tovuti: www.karagwedc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya wilaya,
01 Barabara ya Ikulu,
S.L.P 20,
35482 KARAGWE

*Unapojibu tafadhali taja:KGR/HWK/T.35/15 VOL.I/70*

**TANGAZO LA MNADA** 22.04.2023

Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe inakusudia kuuza Magari na Vifaa chakavu kwa njia ya mnada wa hadhara kama ifuatavyo:

| Aina ya Gari/ Kifaa | Hali yake | Mahali |
|---|---|---|
| Toyota Landcruiser IHZ namba – SM 3492 | Haitembei | Karakana makao makao makuu ya halmashauri |
| Toyota Hilux double cubin namba – STJ 7721 | Haitembei | Karakana makao makao makuu ya halmashauri |
| Toyota Hilux double cubin namba – STJ 7722 | Haitembei | Karakana makao makao makuu ya halmashauri |
| Samani za Ofisi 18,vifaa vya ofisi na tehama, 46 | | Karakana makao makao makuu ya halmashauri |

**Masharti ya Mnada**

1. Malipo sawa na asilimia 25% ya mauzo kulipwa siku mnadani na asilimia 75 kulipwa ndani ya siku kumi na Nne tokea siku ya mnada. Kushindwa kukamilisha na kulipa asilimia 75 kwa muda wa siku kumi na Nne mnunuzi atakuwa amepoteza haki zote na muuzaji atauza mali chakavu upya na asilimia 25 alizolipa hazitarejeshwa.
2. Mnunuzi anatakiwa kuondoa mali aliyonunua ndani ya siku saba kwa gharama zake na kubadili umiliki wa gari na kulipia tozo zote zinazohusika kwa mujibu wa sheria.
3. Mwananchi yeyote anayehitaji kununua gari na vifaa chakavu wanakaribishwa kutembelea eneo vilipo vifaa na gari katika karakana ya Halmashauri siku ya Ijumaa tarehe 28.04.2023 kwa gharama zake.
4. Gari na vifaa vinauzwa kama vilivyo, mnada utaanza saa Nne na nusu Asubuhi (4:30 asubuhi) siku ya Ijumaa ya Tarehe 05.05.2023 katika yadi ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe.

Wote Mnakaribishwa.

Michael F. Nzyungu
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KARAGWE

173939



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
SERA, BUNGE, URATIBU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA)

MAADHIMISHO YA MIAKA 59 YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR


Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan




Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi

Bodi ya Usimamizi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), wanaungana na Watanzia wote kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kutimiza miaka 59 ya Muungano.

***KAULI MBIU: "Miaka 59 ya Muungano Umoja na Mshikamano ndio nguzo ya kukuza Uchumi wetu"***

***"Usalama na Afya Mahali pa kazi huongeza tija" OSHA inasimamia hilo***

Occupational Safety and Health Authority
osha_tanzania_official
TanzaniaOsha
Osha online TV

SIMU YA BURE: 0800110091/2

Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA),
P.O Box 519, DAR ES SALAAM
Simu Na: +255- (0)22 -2760548/276055
Nukushi Na: (022) 27605 Barua pepe: info@osha.go.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Muungano wa Tanzania uenziwe kwa nguvu zote

**LEO** ni Sikukuu ya Muungano. Watanzania nchini kote leo wanaadhimisha miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioundа taifa la Tanzania. Waasisi wa mataifa hayo mawili, walikaa pamoja na kuamua kuziunganisha nchi ili kuwa na taifa moja lenye nguvu kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa watu wote.

Ziko sababu kadhaa zilizowafanya viongozi hao, Mwalimu Julius Nyerere aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Tanganyika wakati huo na Shekhe Abeid Amani Karume, aliyekuwa Rais wa Zanzibar katika kufikia hatua hiyo. Miongoni mwa sababu hizo ni chimbuko la watu wa mataifa hayo kuwa na asili moja, jiografia ya kimaeneo na ulinzi na usalama dhidi ya uvamizi kutoka mataifa ya nje. Lakini sababu kubwa ni kuimarisha uchumi kwa ustawi wa wananchi wa pande zote.

Ikiwa leo Muungano huu umetimiza miaka 59, yako mambo mengi ambayo yameleta manufaa kwa pande zote za Muungano ikiwamo umoja amani na mshikamano katika masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mambo hayo yamesababisha wananchi wa Zanzibar na Tanganyika (sasa Tanzania Bara) kuwa na uhusiano na ushirikiano wa karibu pasina kujali imani, mila na itikadi zao.

Mafanikio makubwa zaidi ni kuendelea kuwapo kwa Muungano huu ambao umekuwa mkongwe kuliko wowote barani Afrika na pengine duniani kote. Ziko baadhi ya nchi Afrika ambazo zilijaribu kuungana lakini zilishindwa. Kwa mantiki hiyo, kuendelea kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ulizaa Tanzania, ni jambo la kujivunia kwa wananchi wake.

Kama wahenga wasemavyo hata vikombe vikiwa kabatini vinagongana, ndivyo ambavyo baadhi ya mambo yamekuwa yakiibuka ndani ya Muungano ama upande mmoja au pande zote husika. Lakini kwa kuwa watu wa pande hizo ndani ya Tanzania ni binadamu na si malaika, hilo ni lazima litokee. Pamoja na hayo ni jambo la kujivunia kwamba kila nyufa zinapojitokeza, zimekuwa zikizibwa kwa maana ya kuwapo kwa maridhiano na hatimaye kusonga mbele.

Mfano hai katika utatuzi wa kero za Muungano ambazo awali zikikuwa 22 lakini tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990, ziliundwa tume mbalimbali ambazo zilikaa na kuzitafutia ufumbuzi. Hadi mwaka uliopita, kati ya kero hizo zilibaki nane ambazo nne kati ya hizo zimepatiwa ufumbuzi na kubaki nne pekee, hali ambayo ni hatua kubwa katika kuhakikisha Muungano unaendelea kushamiri na kustawi.


Mbali na kero hizo, pia kwa nyakati kadhaa ilitokea mipasuko ya kisiasa ambayo ilisababisha kuwapo uhasama wa kisiasa upande wa Zanzibar. Watu walifikia kutokushirikiana katika shida na raha baina ya wanachama na wapenzi wa vyama vikubwa vya CCM na CUF. Hata hivyo, wahenga wanasema wagombanao ndio wapatanao, kwa kutambua hilo, viongozi wa vyama hivyo waliketi na kukubaliana kumaliza tofauti zao na hatimaye kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo awali ilihusisha CCM na CUF na sasa CCM na ACT- Wazalendo.

Licha ya kuendelea kwa Muungano huu, ziko changamoto ndogo ambazo ni sawa na tone la sukari kutokubadilisha ladha ya maji ya bahari. Kwa hiyo changamoto hizo hazina hata nguvu ya kusababisha kuvunjika kwa Muungano.

Kwa ujumla, Muungano uliozaa Tanzania kwa kuunganisha mataifa ya Tanganyika na Zanzibar, una manufaa makubwa sasa kuliko ilivyokuwa mwanzo. Kwa mantiki hiyo kila Mtanzania anapaswa kuulinda kwa nguvu zote badala ya kutaka uvunjike.

Kutokana na umuhimu huo, vijana ambao ndio tegemeo kwa ujenzi na ustawi wa taifa, wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Muungano unalindwa na kutunzwa pamoja na kuwaenzi wasisi wake. Mtu yeyote atakayeanzisha chokochoko kutaka kuvunjika kwa Muungano huu, katu asipewe nafasi na anapaswa kuelezwa ukweli.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Muungano huu Bara na Visiwani unavyoacha hoi kingo za dunia

Na Adam Fungamwango

**TANZANIA** leo inatimiza miaka 59 ya Muungano wa yaliyokuwa mataifa mawili wakati huo, Tanganyika na Zanzibar, yaliyoamua kuacha ubinafsi na kutengeneza taifa moja ambalo kwa sasa linajulikana kwa jina hilo.

Neno Tanzania ni muungano wa majina mawili ya Tanganyika na Zanzibar, ambapo baadhi ya herufi zilichomolewa na kutengeneza jina moja ambalo linatumika hadi leo.

Walikuwa viongozi wa nchi hizo mbili kwa wakati huo, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume walipoamua nchi hizi mbili kuungana Aprili 26, 1964 na jambo hilo baadaye kuthibitishwa na Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi Zanzibar kwenye kilele cha tarehe hiyo.

Siku moja baadaye 27 Aprili 1964, viongozi wa nchi zote mbili walikutana katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam na kubadilishana hati za Muungano.

Mabadiliko ya jina Oktoba 28, 1964 jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lilibadilishwa na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Sheria ya Jamhuri ya Muungano, namba 61 ya mwaka 1964.

Udongo wa Tanganyika na Zanzibar unachanganywa ikiwa ni ishara ya sasa zinakuwa nchi moja. Inawezekana baadhi waliona kama ni mzaha tu hivi, na kwamba baada ya miaka kadhaa mambo yangekuwa tofauti, lakini hadi leo hii umekuwa moja ya Muungano wa kuigwa si Afrika tu, bali dunia nzima.

Muungano wa Tanganyika (sasa Tanzania Bara) na Zanzibar, ndiyo muungano maarufu, bora na imara zaidi dunia kwa sasa ambao hauna mivutano, bali huwa zinajitokeza changamoto za hapa na pale kwa sababu ya mabadiliko ya wakati na mahitaji.

Na mara zote viongozi wamekuwa makini kutatua, ndiyo maana unaendelea kudumu na sasa umefikisha miaka 59 bila kutetereka. Hapa hatuwezi kupita bila kuwashukuru viongozi wa awamu zote zilizopita wa Bara na Visiwani kwa kutoweka maslahi yao binafsi au ya upande mmoja wa muungano, badala yake ya taifa zima la Tanzania.

Maana hapo wala si stori tena au ajabu, kuona mtu wa upande mmoja kwenda upande mwingine, kikazi kwenye kampuni au mashirika ya kiserikali na kibinafsi. Hata majeshi yetu ni moja, askari wa bara anakwenda kufanya kazi Zenji, na wa Zanzibar anakwenda Bara.

Kwa sasa Watanzania wameshazoea kabisa kuona hata kiongozi wa Zanzibar anakwenda anakwenda kuongoza Zenji, kwenye nyanja mbalimbali kichama na kiserikali, na hata wa Zanzibar, pia anawaongoza Bara, au kuongoza watu wote pande zote mbili akiwa anatoka upande wowote wa Muungano.

Ndani ya kawaida, inaonekana kama ni jambo dogo, rahisi na la kawaida, lakini hili limetengenezwa vichwani na Watanzania na waasisi waliopita, si rahisi kulikuta jambo hili kwenye baadhi ya nchi duniani.

Tangu Muungano uanze hadi kwenye miaka ya 1980, kulikuwapo hangamoto nyingi ya Watanzania Bara kwenda Zanzibar na kitambulisho, lakini baadaye lilitatuliwa na nadhani katikati au mwishoni mwa miaka ya 1980, wananchi wa Tanzania Bara wakaanza 'kutimba' Zenji, bila pasipoti kwa sababu hakukuwa na umuhimu wa kitu hicho tena, wote ni Watanzania.

Nadhani awali ilipaswa kuwa hivyo kwa sababu za kiusalama, kwani ndiyo kwanza Muungano ulikuwa mchanga na wapo maadui ambao hawakupendezwa na hilo.

Novemba mwaka jana kero ya bidhaa kutoka Zanzibar kulipiwa ushuru uliokuwa unalalamikiwa, imepatiwa ufumbuzi na sasa mambo ni mazuri.

Kusema kweli Muungano huu ndiyo moja ya vitu maalumu, ambavyo vinaiweka Tanzania kwenye ramani ya nchi za mfano wa kuigwa duniani, kwani hata baadhi ya nchi ambazo zimejipambanua kuwa kubwa na zenye demokrasia zimeshindwa.

Kwa maana hiyo, viongozi waliopo waendelee kuuenzi Muungano huu kwa gharama yoyote ile. Najua bado zipo changamoto na zitaendelea kuwepo kwa sababu haziepukiki kutokana na kile nilichokibainisha, wakati na mahitaji ya muda husika.

Nadhani wadau, wananchi na wanasiasa watakuwa wanaziainisha kila zinapojitokeza, lakini pia hili la Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), na Shirikisho la Mpira na Miguu Zanzibar (ZFF), ni moja kati ya kero zinazotakiwa kufanyiwa kazi pia.

HABARI KITAIFA

# Treni mwendokasi Dar - Moro mguu sawa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeshafanya majaribio ya vituo vyote vya Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es salaam hadi Morogoro na kwa sasa vinasubiriwa vichwa vya treni ya mwendokasi vinavyotarajiwa kuwasili mwezi ujao huu ili kuanza safari.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mbulu Mjini (CCM), Zacharia Issaay.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema huduma ya treni ya mwendokasi nchini inasubiriwa kwa hamu kubwa sana na kuhoji lini itaanza kutolewa kati ya Dar es salaam na Dodoma.

Akijibu swali hilo, Mwakibete alisema awamu ya kwanza itaanza kutoa huduma Dar es Salaam na Morogoro.

"Hivi ninapozungumza tumeshafanya majaribio kwenye vituo vyote na treni ya mkandarasi. Kwa sasa tunasubiri vichwa vije na vitakuja ndani ya Mwezi Mei ili ianze kufanya kazi hii SGR," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Mlimba (CCM), Godwin Kunambi, alihoji lini vituo vidogo vya treni vya Njagi na Itongowa katika reli ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) vitarejeshwa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema serikali kupitia TAZARA ilipokea maombi ya kufunguliwa kwa vituo vidogo vya Njage na Mtongowa katika vipindi tofauti mwaka 2022.

Alisema baada ya kufanya tathmini, ilibainika kwamba kituo kidogo cha Njage kinachoombwa kufunguliwa kipo katikati ya kituo kikubwa cha Mngeta na Mbingu ambapo treni za abiria husimama.

"Umbali kati ya Mngeta na Mbingu ni kilometa 18 na kituo cha Njagi kiko katikati yaani kilometa tisa kutoka kila upande. Kuhusu kituo cha Mtongowa, hiki kiko kati ya kituo kikubwa cha Chita na Mngeta ambapo tayari kuna kituo kidogo cha Ikule ambacho treni za abiria husimama. Aidha, umbali kati ya Chita na Mngeta ni kilometa 16 na kituo kidogo cha Mtongowa kipo kilometa tisa kutoka kituo kikubwa cha Mngeta,"alisema.

Alisema ili uendeshaji wa treni uwe wenye ufanisi, usafiri wa reli za masafa marefu unashauriwa uwe na vituo vyenye umbali usiopungua kilometa 20 kutoka kituo kimoja hadi kingine.

Aidha, alisema vituo vilivyoombwa kurejeshwa vipo chini ya nusu ya umbali unaoshauriwa kwa treni za masafa marefu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa elimu nje ya nchi Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel (kushoto), akitoa maelezo kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na wakala huo kwa ujumbe wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), uliotembelea ofisi za wakala Chang'ombe, Dar es Salaam juzi, baada ya kusaini mkataba wa kutafuta fursa nje ya nchi. Wa pili kushoto ni Mkuu wa taasisi hiyo, Prof. William Pallangyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Uwekezaji fya wakuza matibabu ya kibingwa

**Na Mwandishi Wetu**

JITIHADA za Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kuna upatikanaji wa vifaa bora vya matibabu pamoja na kukarabati miundombinu ya hospitali unaofanywa wa serikali, zimesaidia kukuza matibabu ya kibingwa.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Upasuaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) Tawi la Mloganzila, Dk. Godlove Mfuko, wakati akizungumzia huduma za kibingwa zinazotolewa hospitalini hapo.

Alisema jitihada na maelekezo ya Rais Samia yaliyotekelezwa kikamilifu yamesaidia huduma za afya kuboreshwa na kupunguza idadi ya Watanzania wanaokwenda nje ya nchi kutafuta huduma za kibingwa.

"Ukiona sasa unasikia serikali inawekeza pia katika kusomesha madaktari bingwa katika hospitali zetu bila kusahau wingi wa vifaa bora katika hospitali zetu haswa hii ya Mloganzila, ni sababu ya kwanza ya sisi wataalamu kutoa matibabu mazuri kwa wagonjwa.

"Sisi kama wataalam au madaktari bingwa wabobevu, tunachukua jambo hili kama moja ya mambo mengi mazuri yanayofanywa katika kipindi cha utawala wa Rais Samia," alisema Dk. Mfuko.

Alisema serikali imenunua vifaa bora vya kufanyia uchunguzi wa magonjwa mbalimbali kiasi cha kuwafanya wataalamu wa afya nao wajikite kutafuta suluhu ya changamoto za matibabu.

"Mfano mzuri mpaka sasa tumeshafanya upasuaji wa wagonjwa zaidi ya 100 waliokuja kwa ajili ya kupunguza uzito kwa kupandikizwa (puto) na huduma hiyo imefanikiwa kwa asilimia 100.

"Kama hiyo haitoshi hospitali yetu ya Mloganzira imefanya upasuaji wa kipekee wa kupandikiza figo kwa wagonjwa watatu kwa utaalamu wa tundu dogo, ikiwa ni teknolojia ya aina yake isiyoacha maumivu makali kwa mchangiaji na yule anayechangiwa pia, huduma ambazo haziwezi kufanikiwa kama serikali haijanunua vifaa vya kisasa pamoja na kuweka miundombinu mizuri," alisema.

Dk. Mfuko alisema sekta ya afya Tanzania imekua kwa kiasi kikubwa, hali inayoleta sifa kwa serikali na Taifa, huku akisema kuna uwezekano mkubwa nchi itaanza kupokea wageni kutoka mataifa mbalimbali kuja kupata huduma ya matibabu nchini.

Alisema taifa lolote linalowekeza pia kwenye afya lina asilimia kubwa la kukuza uchumi wake, kwa sababu mtu anayeugua, hawezi kufanya kazi za kimaendeleo, ukizingatia kuwa baadhi ya magonjwa ni ghali na yenye kutumia muda mwingi.

"Watanzania ni mashahidi kuwa miaka michache iliyopita, watu walikuwa wanasafiri nje ya nchi na kutumia gharama kubwa kufuata matibabu ya kibingwa kama figo, moyo na mengineyo, lakini sasa yanapatikana nchini, hii yote ni kwa sababu serikali imeamua kuboresha sekta hii muhimu," alisisitiza Mfuko.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# TOSCI yateketeza tani 356 za mbegu feki

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), imeteketeza tani 356 za mbegu zisizokidhi ubora katika kukabiliana na mbegu feki nchini katika kipindi kati ya mwaka 2020 na 2022.

Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Dk. George Swela, alisema jana kuwa mbegu hizo zimeteketezwa kwa sababu ya kutofikia kiwango cha uotaji na kusinyaa kupita kiasi.

Dk. Swela alizitaja aina za mbegu zilizoteketezwa mwaka 2020 kuwa ni za mboga mwaka 2021 waliteketeza jumla ya tani 289 ambazo ni mahindi tani 219, choroko tani moja, mpunga tani moja, mtama tani 12 na alizeti tani sita.

Alisema mwaka 2022 waliteketeza jumla ya tani 58 za mbegu ambazo ni alizeti tani 22, mahindi tani mbili, viazi Mviringo tani 29 na mtama tani tano.

Dk. Swela alisema licha ya kuteketeza mbegu hizo, tayari kesi saba zinaendelea katika mahakama mbalimbali nchini dhidi ya waliokamatwa na mbegu hizo na kwamba wahusika watahukumiwa kulingana na makosa yao mara watakapopatikana na hatia kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Alifafanua kuwa mwaka 2021 kesi tano zilifikishwa mahakamani katika mikoa ya Ruvuma wilayani Mbinga, Songwe wilayani Momba na Mbeya wilayani Mbeya na Rungwe.

Dk. Swela alisema mwaka 2022, kesi mbili zilifikishwa mahakamani katika mikoa ya Mbeya wilayani Mbeya.

Alisema TOSCI hufanya ukaguzi na wanapobaini kwamba kuna mbegu iliyokwisha muda wake na bado iko kwenye maghala au dukani, huwaagiza kuziteketeza na wanaposhindwa kufanya hivyo, taasisi husimamia uteketezaji kwa maslahi yao na taifa kwa ujumla.

Dk. Swela alisema wameweka mikakati ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza mara kwa mara kwenye maduka na maghala ili kukomesha suala la mbegu feki au zisizo na ubora ambazo zikipandwa zinaweza kutoota au zikaota, hutoa mazao yasiyolingana na maelekezo yaliyomo kwenye nembo na kumsababishia mkulima kupata hasara.

Mkaguzi wa Mbegu kutoka TOSCI, Fatuma Nasoro, alisema taasisi hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa mawakala wote wa mbegu kabla hawajaanza kufanya biashara ili kujua sheria zake ikiweao kuwa na matumizi ya nembo ya TOSCI kuashiria mbegu inayouzwa imekidhi viwango vyenye ubora.

Alisema elimu hiyo pia inahusu kubaini mbegu zenye ubora zinazopaswa kuuzwa kwa mkulima na sizizo na ubora (mbegu feki) ambazo hazikidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa kulingana na sharia, kanuni na miongozo kutokana na Sheria ya Mbegu ya Tanzania ya mwaka 2003 na kanuni zake.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo akiwajulia hali baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kipaumbele, waliojeruhiwa na radi wakiwa darasani wanafanya mtihani na kulazwa katika hospitali ya wilaya hiyo, jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Mwanafunzi kidato cha nne afariki dunia akiwa kwenye mtihani

**Na Steven William,** NACHINGWEA

MWANAFUNZI wa Kidato cha Nne katika Shule ya Sekondari ya Kipaumbele, Nachingwea mkoani Lindi, Alex Justine (18) amefariki dunia baada ya kupigwa na radi.

Justine alikumbwa na mauti juzi akiwa darasani akifanya mtihani wa kujipima (Mock) kwa ngazi ya wilaya. Sambamba na kifo hicho, wanafunzi wengine 44 walijeruhiwa katika tukio hilo.

Akithibitisha kutokea kwa kifo hicho, Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo, alisema ni kweli radi imesababisha kifo cha mwanafunzi huyo huku pia akibainisha wanafunzi wengine 44 kujeruhiwa.

Hata hivyo, Moyo alisema wanafunzi wa kike waliojeruhiwa wanaendelea vizuri huku majeruhi wa kiume 11 wakiwa katika hali nzuri lakini mmoja alifariki dunia kabla ya kufikishwa Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya, Dk. Ramadhan Maige, alisema majira ya saa 9:30 alasiri alipokea simu kutoka kwa ofisa elimu sekondari juu ya kutokea kwa ajali iliyotokana na radi.

Dk. Maige alisema kuwa walipokea majeruhi 45 kutoka katika Shule ya Sekondari Kipaumbele huku mwanafunzi mmoja akiwa tayari ameshafariki dunia.

# TIA, GEL zaingia mkataba Watanzania kusoma vyuo vya nje

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Uhasibu Tanzania (TIA), imetia saini mkataba na Wakala wa Vyuo Vikuu Nje ya Nchi (Global Education Link - GEL) ili kushirikiana kuitafutia taasisi hiyo fursa za wanafunzi na wahadhiri kwenye vyuo vikuu vya nje.

Mkataba huo ulitiwa saini jana kwenye ofisi za GEL, Chang'ombe, Dar es Salaam kati ya , baina ya Mkurugenzi Mtendaji wa GEL, Abdulmalick Mollel na Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Profesa William Pallangyo.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Mollel alisema GEL kwa miaka 16 imekuwa ikisaidia watanzania wanaotaka kwenda kusoma nje ya nchi kuanzia ngazi ya cheti, stashahada, shahada, shahada za uzamili na za uzamivu ili kutimiza ndoto zao kwenye taaluma wanazozipenda.

Mollel alisema jukumu lingine la GEL ni kuishauri serikali inapoona fursa zilizoko nje ya nchi ambazo haziko hapa nchini namna watanzania wanavyoweza kunufaika na fursa hizo.

Alisema wamekuwa wakisaidia kutengeneza ushirikiano kati ya vyuo vikuu vya nje ya nchi na vya ndani ya nchi na kwamba kabla ya kufanya hivyo lazima GEL iwe na makubaliano na chuo kinachotaka kuunganishwa na zaidi ya vyuo vya nje 300 wanavyofanya kazi navyo.

GEL, alisema itashirikiana na TIA kupata mikataba yenye tija na vyuo vikuu vya nje kuanzia kwenye kupata ufadhili wa masomo kwa wahadhiri wake kwenda kusoma ngazi ya shahada za uzamili au za uzamivu.

"Tunatamani kuona vyuo vikuu vyetu vinakuwa na kozi ambazo zinaweza kushirikiana na vyuo vya nje kwa kusoma miaka miwili hapa nchini na kwenda kumaliza kwenye vyuo vya nje kwa kutumia mitaala ya hapa nchini au mitaala ya nje ya nchi na hii itasaidia sana sisi kupata wanafunzi wa kimataifa kuja kusoma hapa kwetu," alisema Mollel.

Alisema vyuo vikuu vingi duniani vinafanya mikutano ya kimataifa ambapo wahadhiri wa vyuo vya ndani wanaweza kushirikiana na wahadhiri wa vyuo hivyo kutoa machapisho mbalimbali kwa pamoja na kutoa mafunzo ya pamoja kwa wanafunzi wa vyuo vyao.

Mikataba kama hiyo, alisema itasaidia kuvitambulisha vyuo vikuu vya Tanzania kwenye mataifa mbalimbali ili wanafunzi wa nchi hizo wajue kozi zinazotolewa na kuja kusoma hapa nchini.

"Leo hii kuna maonyesho ya zaidi ya vyuo vikuu 200 nchini China ambavyo vina fursa za kutosha kwa hiyo vyuo vikuu vyetu navyo vinapaswa kushiriki maonyesho kama haya kuvutia raia wa mataifa hayo kusoma kwenye vyuo vyetu," alisema.



Mollel pia alisema mkataba huo utakiwezesha chuo hicho kubadilishana wanafunzi na vyuo vikuu vya nje kwa wanafunzi wake kusoma hapa nchini nusu ya muhula na kwenda kumalizia nje ya nchi na wale wa nje ya nchi kuja kumaliza muhula wao hapa nchini.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Prof. William Pallanyo, alisema mwaka huu taasisi hiyo nafikisha miaka 50 ikiwa inafundisha masomo ya uhasibu, rasilimali watu, ununuzi, masoko kwenye kampasi sita za Dar es Salaam, Singida, Mwanza, Mbeya, Kigoma na Mtwara na kwamba mwakani wanatarajia kuanzisha kampasi visiwani Zanzibar.

Alisema GEL imekuwa ikiwasaidia wanafunzi wa Tanzania kupata vyuo vya kujiendeleza nje ya nchi hivyo kuingia mkataba nayo kutatoa fursa kubwa kwa TIA kutoa mafunzo ya kimataifa kwa wanafunzi wa chuo hicho kupata nafasi ya mafunzo kwenye vyuo ambavyo watashirikiana kupitia GEL.

"MoU hii ni fursa nzuri kwa wanafunzi na wahadhiri wetu kupata vyuo vikuu vya kujiendeleza nje ya nchi ka wale wanaotaka kusomea Shahada ya Uzamili na Shahada za Uzamivu na tutapata fursa ya kupata machapisho kwenye maktaba za wenzetu nje ya nchi.

"Hii itawapa fursa vijana wetu kukua kadri teknolojia inavyozidi kukua duniani kwa sababu teknolojia inabadilika kwa haraka sana kwa hiyo tukiendelea kujifungia ndani uwezekano wa kwenda na kasi ya wenzetu tutakuwa tumechelewa, baada ya kusaini hapa tutaanza kufanya yale yote yaliyotajwa kwenye mkataba huu," alisema.



# MIAKA 59 YA MUUNGANO

# Nafsi na siasa zake Rais Dk. Samia, zinavyoshikamana na Muungano hai



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

LEO ni siku mahsusi ikisherehekewa miaka 59 ya mvumo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais aliyepo ni Dk. Samia Suluhu Hassan. Pengine, mchambuzi au mdadisi wa kisiasa anaweza kujiuliza namna anavyofungamana na tukio hilo?

Kimsingi, inabeba kama walivyo wachambuzi na wataalamu wote wa sayansi ya siasa, wanajikita katika uhalisia wa siasa, pia nafsi yake binafsi mkuu huyo.

Rais Dk. Samia leo akitumikia nafasi hiyo ofisi yake ikiwa upande wa bara, mzizi wake ni mzaliwa wa Visiwani Zanzibar, alikosoma shule hadi kufunga ndoa yake. Hata hivyo, alivyojiunga na ngazi ya chuo, akaangukia kunufaika na duru za Muungano walizoanzisha watangulizi wake wastani muongo mmoja kabla, akijiunga na Chuo cha Uongozi wa Maendeleo (IDM) - Mzumbe, vilevile Chuo Kikuu Huria (OUT), miaka nane iliyopita.

Ukirejewa mzizi wa uzoefu wa ajira yake hadi kujitosa siasa, Dk. Samia ameipatia Zanzibar, hususan Unguja alikozaliwa, akachipua kuanzia mwaka 2,000 alipojiunga rasmi kwenye siasa hai, akigombea ubunge wa viti maalum kwa bendera ya CCM na akaipata nafasi hiyo.

Hapo akamea zaidi kisiasa, pale Rais wa Zanzibar wakati huo, Amani Abeid Karume, alipomteua kuwa Waziri wa Utalii na Biashara, katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ). Akarejea tena kwenye uchaguzi wa mwaka 2005, akachaguliwa tena kwenye viti maalum na ilipoundwa Baraza Mawaziri, yeye akakabidhiwa Wizara ya Kazi, Jinsia na Watoto ndani ya SMZ. Hadi kufika mwaka 2010, Samia alikuwa na uzoefu wa kutosha miaka 10 katika siasa na nafasi hizo.

> Hadi kufika Aprili 30 2021, akawa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa chama tawala - CCM, katika ukanda wote wa Muungano.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ally Mwinyi

Hapo Mama Samia, katika kile kiliendana na wito uliokwishatolewa awali ndani ya CCM huko nyuma kwamba kinamama wanaopitia viti maalum, ni vema wakafanya maboresho wakijitosa kuwania viti majimboni, naye akafanya hivyo kupitia jimbo la Makunduchi Unguja, akatwaa nafasi, safari hiyo ikiwa ni ya Bunge la Muungano.

Kwenye matokero hayo, jimbo la Makunduchi na akafanikiwa kupata ushindi wa kishindo wastani wa asilimia 80, ukimpa jukumu la kuvuka bahari kwenda kuhudhuria vikao vya Bunge Tanzania Bara, jijini Dodoma, nyum aya pazi akiwa na uzoefu wa kutosha kuwajibikia wizara za kibishara, utalii, jinsia, kinamama, watoto na ajira.

Rais Jakaya Kikwete, wakati huo akiwa katika awamu ya pili ya uongozi wake, akavutiwa naye, hata kumuweka kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, anayeshughulilikia Muungano. Hapo nako kukawa wigo uliotamnua zaidi na mambio yanahusu Muugano, hata Mazingira.

Ilipofika mwaka 2014 kuibuka Bunge Maalum la Katiba, Dk. Samia aloshaiva mno hata akakasimiwa kuwa Makamu Mwenyekiti, ikiwa lina na sura ya Muungano, kukitawaliwa mjadala wa dai la katiba mpya ya nchi, jambo ambalo hadi sasa halijamtoka 'mkononi' kukisikia michakato mbalimbali anayoenda nayo hadi leo.

Sura moja ya utekekezaji wake inashuhudiwa hivi karibuni, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo jijini hapa, akasema mchakato wa Katiba mpya unatarajiwa kuanza kufanyiwa kazi baada ya kupitishwa bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Historia ya heshima na neema ya kiuongozi katika picha ya Muungano, ikaendelea kudumu kwa Dk. Samia alipopanda daraja daraja kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Dk. John Magufuli, kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 na hata baada ya ushindi, akawa rasmi Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Kimsingi, alipanda daraja katika ofisi aliyotumikia akiwa waziri, wajibu mpya akiwa mwelekezaji na msimamizi mkuu wa masuala ya Muungano na Mazingira, pia Msaidizi Mkuu wa Rais, alikodumu kwa muhula na hata baada ya uchaguzi uliofuata mwaka 2020, akabaki kwenye nafasi hiyo kwa wastani wa mwaka mmoja, hadi kilipotokea kifo cha Rais Dk. Magufuli, akakasimiwa urais kwa mujibu wa katiba.

Hadi kufika Aprili 30 2021, akawa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa chama tawala - CCM, katika ukanda wote wa Muungano.

Mbali na kutumikia nafasi hiyo ya juu, kusimamia mihimili ya Muungano kwa chama tawala, hadi serikali, katika familia yake ameunda zao la kuwa na binti, anayechipukia kwa njia zake, akiwa Mbunge wa Viti Maalum ndani a Bunge la Jamhuri ya Muungano.

**HISTORIA YA NCHI**

Rais Dk. Samia katika historia ya nchi, ana jingine kwamba ni rais wa pili kutoka upande wa Zanzibar, tangu kupatikana Muungano mwaka 1964, akitanguliwa na Mzee Ali Hassan Mwinyi, aliyestaafu miaka 26 kabla ya urais wake, 1995.

Kingine cha kihistoria kitaifa na kimataifa kuanzia na ulingo wa Muungano, Jumuiya ya Afrika Mashariki na hata anga za mbali akaonyesha kuwa "Rais mwanamama anayeweza kwa vitendo akiweka rekodi ya kazi kadhaa kimataifa ndani ya miaka miwili," ikiwa na mrejesho wa sifa za Muungano.

Leo hii, Rais Dk. Samia katika sura nyingine ana zawadi kubwa ya kijinsia anakionyesha kutetea kinamama katika timu ya Muungano, kuanzia safu yake ya Baraza la Mawaziri ikisheheni timu ya 'kinamama wanaoweza', hadi nyenzo za wateule wake wanaongoza mikoa na wilaya wakishamiri kinamama, pia historia kwa baadhi ya wizara kama Ulinzi, kwa mara ya kwanza kuongozwa na mwanamama.

Hilo linaendana kutosahau kada ya vijana, ambayo alitangaza wazo kwamba ndio anawapa nafasi hata katika upande wa timu ya Baraza la Mawaziri.

TANGAZO

# MIAKA 59 YA MUUNGANO, HUDUMA YA MAJI IMEKUWA IMARA

NA MWANDISHI WETU

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umeimarisha zaidi Sekta ya Maji katika miaka 59. Jambo hili kwa umri wa Muungano lipo wazi kwa kazi mbalimbali zinazofanywa na wataalamu wa Sekta hii muhimu katika jamii yetu.

Kazi ya huduma ya maji kwa jamii ni baraka. Maji ni rasilimali muhimu kwa maisha ya binadamu, maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, rasilimali za maji ni kichocheo muhimu katika shughuli za majumbani, kilimo cha umwagiliaji, mazingira, umeme wa nguvu za maji, viwanda, uvuvi, mifugo, madini na utalii. Upatikanaji wa maji kwa ajili ya sekta mbalimbali pamoja na usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji ni msingi wa shughuli zote za maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa usalama wa Taifa.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), anayeongoza jambo hili muhimu katika jamii, akiongea na mwandishi wa makala hii hivi karibuni amesema Serikali ya awamu ya sita, imejipambanua katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama vijijini na mijini unazidi kuimarika.

Vijijini upatikanaji wa maji umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwaka 2021 hadi asilimia 77 mwezi Februari 2023. Pia. upatikanaji wa huduma ya maji kwa upande wa mijini umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 84 mwaka 2021 hadi wastani wa asilimia 88 mwezi Februari 2023" Mhe. Aweso amesema.




*Moja ya magari yenye mitambo ya kuchimba maji chini ya ardhi yaliyonunuliwa na Serikali katika kuhakikisha huduma ya majisafi na salama inawafikia Watanzania, magari hayo yamenunuliwa na Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19.*

Ameongeza kuwa hatua hiyo ni azma ya Serikali ya Awamu ya sita katika kuwapatia wananchi majisafi, salama na yenye kutosheleza, pia kujitoa kwa viongozi kwa nia madhubuti ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani.

Mhe. Aweso ameainisha kuwa katika kuhakikisha kiwango cha upatikanaji maji kwa wananchi kinaongezeka, kazi mbalimbali zimefanyika katika sekta ya maji kwa ushirikiano kati ya viongozi, wananchi na wataalamu wa sekta ya maji ambao hushirikiana kwa pande zote mbili za muungano katika kazi.

Miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na kutekelezwa kwa jumla ya miradi 218 ya mijini na vijijini yenye uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao milioni 2.09 kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) katika kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19.

"Sanjari na hilo kukamilika kwa jumla ya miradi 1,197 ya usambazaji maji na kutoa huduma kwa wananchi waishio katika vijiji 2,056 nchini ambapo jumla ya Shilingi 401,544,508, 623.00 zimetumika kugharamia miradi hiyo" Mhe. Aweso amesema na kuongeza kuwa kukamilika kwa miradi hiyo kunafikisha jumla ya vijiji 9,144 vyenye huduma maji nchini. Pamoja na hilo, miradi 150 imeanza kutoa huduma kati ya miradi 177 iliyokuwa na changamoto ya utoaji huduma kwa muda mrefu kwa wananchi (miradi chechefu).

Ameainisha kuwa utekelezaji wa programu ya Malipo kwa Matokeo (maarufu kama PforR) umefanyika kwa ufanisi na kuwezesha kuongezeka kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini kutoka Dola za Marekani milioni 350 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 650.

Kuhusu ubora wa maji ameweka bayana kuwa nchi ya Tanzania hivi sasa inazo maabara zenye Ithibati na zinaweza kufanya kazi mahali popote hapa Duniani. Maabara za ubora wa maji nchini zenye Ithibati nchini zimeongezeka kutoka moja (Mwanza) mwaka 2021 hadi 7 za Singida, Shinyanga, Kigoma, Bukoba, Musoma na Dar es Salaam; Pia mtandao wa maabara za ubora wa maji nchini umeongezeka kutoka 16 mwaka 2021 hadi kufikia 17 mwezi Februari 2023 kutokana na kuanzishwa kwa maabara ya ubora wa maji ya mkoa wa Manyara.

Mhe. Aweso amesema kiu imejibiwa ya kuona miradi iliyosubiriwa kwa muda mrefu na wananchi ambapo Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka miwili imeanza utekelezaji. Mosi akitaja kusainiwa mikataba na kuanza ujenzi wa miradi ya maji katika miji 28 iliyokwama kwa muda mrefu na inaendelea na utekelezaji; pili kusainiwa kwa mkataba na kuanza ujenzi wa bwawa la Kidunda litakalokuwa suluhisho la upungufu wa maji katika mto Ruvu ambao ni chanzo kikuu cha maji katika mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani.

Jambo la tatu kuhusu ujenzi ni kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bwawa la Farkwa ambalo ni tegemeo la utatuzi wa changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika jiji la Dodoma na miji ya Bahi, Chemba na Chamwino ambapo hadi mwezi Februari 2023 fidia kwa wananchi wanaopisha mradi imetolewa na taratibu za manunuzi kwa ujenzi zimeanza.

Mhe.Aweso anasema vifaa vya kisasa vya kutoa huduma katika Sekta ya Maji vimenunuliwa ili Watanzania wapate huduma ya maji ya uhakika wakati wote. Amesema vifaa hivyo vimenunuliwa na kuanza kutumika ikiwamo seti 25 za mitambo ya kuchimba visima, seti tano za mitambo uchimbaji na ujenzi wa mabwawa na seti nne za vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi.

Ni hakika kuwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa Sekta ya Maji imeweka jitihada kubwa kwa kutekeleza kazi mbalimbali, ili kuwahudumia wananchi, zilizotajwa ni baadhi kati ya kazi nyingi.

Lengo la Serikali husan katika Sekta ya Maji ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi waishio vijijini unafikia zaidi ya asilimia 85 na zaidi ya asilimia 95 kwa mijini. Ni wazi kwa mipango iliyopo na kazi zinazoendelea mambo mazuri zaidi kwa wananchi bado yanakuja ilikuimarisha huduma ya maji katika jamii.

173909

AWAMU YA SITA NA KERO...

# Wasomi & wanasiasa katika butwaa la kasi, miaka miwili zimeondoshwa 15

**Na Sabato Kasika**

HADI sasa Dk. Samia Suluhu Hassan, ana miaka miwili akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania. Kuna mengi katika ukanda huo wenye historia ya miaka 59 unaotimu leo, kwa milima na mabonde ya kuwajibikia umma huo.

Mchambuzi wa siasa, Abbas Mwalimu, anasema katika kipindi cha miaka miwili pekee hadi kufika sasa, serikali ya awamu ya sita imefanikiwa kutatua zaidi ya hoja 15 za Muungano, akitamka: "Hayo ni mafanikio makubwa katika Muungano wetu, kwani kipekee, katika kipindi cha miaka miwili tu, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, tumeshuhudia idadi hiyo ya hoja zikitatuliwa."

Ni juzi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo akasema bungeni kuwa katika mwaka wa fedha unaoisha 2022/23, ofisi yake iliratibu vikao vitatu vya kujadili masuala ya Muungano, kwamba hoja nne kati ya nane zilizojadiliwa zilipatiwa ufumbuzi.

Dk. Jafo anazitaja hoja hizo ni: Malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, kodi ya mapato (PAYE) na kodi ya zuio; mkataba wa mkopo wa fedha za mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume; na ongezeko la gharama za umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenda Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO).

Anasema kamati ya pamoja ya Serikali ya Muungano na ile ya Mapinduzi (SMZ), ziliwashirikisha mawaziri na makatibu wakuu husika.

Waziri Jafo anasema hoja ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili, ilitokana na kuwapo tofauti za ukadiriaji viwango vya thamani za bidhaa na kodi ya forodha baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, inayosababisha kulipa kodi ya ziada zinazotoka Zanzibar kwenda katika soko la Tanzania Bara.

Jafo anasema ufumbuzi wa hoja hiyo ulipatikana baada ya kubainika uhalisia wake na sasa linaeleweka vizuri kwa wafanyabiashara wa Zanzibar wanaopeleka bidhaa bara.

Kwenye ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Jafo anasema shida ilikuwa kuchelewa kutiwa saini mkataba wa mkopo kati ya serikali na Benki ya Exim ya China, baada ya mkataba kuhusisha vipengele vya kuweka mali za serikali kama dhamana ya mkopo.

Anasema, ufumbuzi ulipatikana baada ya Serikali ya Muungano kukubali kuondoa sharti hilo, hivyo kuwezesha mkataba wa mkopo huo kutiwa saini mnamo Novemba mwaka jana.

Kuhusu gharama ya umeme, akafafanua kwamba shida imekuwa kuongezeka bei ya umeme kwa wateja wa TANESCO ikiwamo Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO).



Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, wa Tangayika alipobadilishana hati za Muungano na Shekhe Abeid Aman Karume wa Zanzibar. **PICHA: MAKTABA.**

**HISTORIA ILIKOTOKA**

Mchambuzi Abbas anafafanua kuwa tangu kuanzishwa Kamati ya Pamoja ya Kushughulikia Masuala ya Muungano mwaka 2006, kuna jumla ya hoja 25 ziliibuliwa na kufikia mwaka 2021 hoja 18, zilishajadiliwa na kupatiwa ufumbuzi na kuondolewa katika orodha ya hoja za kero za Muungano.

"Hoja nyingine nne zilipatiwa ufumbuzi katika kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ cha Disemba 6, 2022, hivyo jumla ya hoja zilizopatiwa ufumbuzi na Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ni 22," anasema.

Abbas, anataja baadhi ya hoja hizo zilizopatiwa jina 'kero za Muungano' kuwa ni: Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; utekelezaji wa Sheria ya Usafirishaji Majini; Uwezo wa Zanzi-

INAENDELEA UK. 15

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)



MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MHE. DKT. HUSSEIN ALI MWINYI
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

MIAKA 59 YA MUUNGANO

Mwenyekiti, Makamishna, Menejimenti na Wafanyakazi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC),wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi na Wananchi wote katika kuadhimisha miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

'Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi'




173934

Mrajis wa Vyama vya Ushirika,, S.L.P 201,Dodoma,Mtaa wa Kuu,, Simu +225262322993,
Barua pepe:ushirika@ushirika.go.tz, Tovuti: www.ushirika.go.tz
Ushirika_tcdc
Tume ya Maendeleo ya Ushirika

**TANGAZO**


SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR**

# MAFANIKIO YA SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR NA MIAKA 59 YA MUUNGANO

Shirika la umeme Zanzibar(ZECO) lilianzishwa kwa sheria no 3 ya mwaka 2006.lakini kabla ya hapo lilikuwa likijulikana kama shirika la mafuta na nguvu za umeme lilianzishwa wakati wa mapinduzi ya mwaka 1964.

Katika kusherekea maadhimisho ya miaka 59 ya sherehe za muungano tunaendelea kushuhudia mafanikio makubwa tangu Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya mapinduzi ya Awamu ya nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi zilipoingia madarakani. Katika serikali hii ya awamu ya nane kupitia ilani ya chama cha mapinduzi kabla ya kufikia 2025 serikali kupitia shirika la umeme Zanzibar(zeco) litaingiza kwa mara ya kwanza uzalishaji wa umeme mara ya kwanza kupitia nishati ya jua.mradi mkubwa unaofadhiliwa na bank ya dunia ,

Akizungumza na gazeti la nipashe ofisini kwake Gulioni Zanzibar, Khamis Ame Mnubi,Afisa habari wa shirika hilo anasema, " kuna faida nyingi walizopata kupitia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar"

Faida kubwa ni kuongeza mashirikiano kati ya ZECO NA TANESCO.Mashirikiano makubwa yanakuja kwasababu umeme tunaotumia Zanzibar unatoka Tanzania bara. Na TANESCO ndiyo wanaouza umeme huo.chanzo cha kusambazia umeme huo kipo Tanzania bara kilomoni,pamoja na Tanga majani mapana kwa umeme unaokwenda pemba. Tanesco wamekuwa wakitoa ulinzi na msaada pindi dharura inapotokea

Pia faida nyiongine ni ushirikiano wa kiufundi endapo kunapotokea itilafu za kukosekana kwa vifaa vya kiufundi. Hasa katika eneo la mtoni ambalo ndilo eneo kuu la kusambazia umeme."huwa tunawapigia Tanesco na mara nyingi wamekuwa wakitoa msaada."

Faida nyingine kubwa ya Muungano ni kupitia uongozi wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kupita fedha za uviko 19 zaidi ya Billion 11 ambazo zilielekezwa moja kwa moja kumsaidia mwananchi wa Zanzibar. Ili kumpungumzia gharama za kusambaziwa na kuungiwa umeme. Lakini kupitia pia Tamko la raisi wa Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar dkt Hussein Ali Mwinyi anasema," mwananchi yoyote wa Zanzibar ataweza kusambaziwa nguzo za umeme bure tofauti na hapo awali". Hayo ni matunda yatokanayo na Muungano huu.

Akizungumzia muelekeo wa Shirika la umeme Zanzibar (ZECO)anasema wanaangalia vyanzo vingine mbadala vya umeme ,"wamejikita pia katika kuangalia nishati ya umeme wa jua kupitia mradi mkubwa wa ZESTA Ambao tayari umeshaanza kwa hatua katika eneo la Makunduchi. Hatua za awali tayari zimeshafanyika.kwa sasa wanasubiri mtaalamu elekezi ili hatua nyingine ziweze kuendelea.

Mradi huu utaweza kuzalisha mega watt 10-15 za umemeambazo nazo zitaingizwa katika gredi ya Taifa. Ili kuongeza mega watt 100 ambazo zinatumika kwenye line mpya na vilevile zile 40 kwenye line kongwe

Pia wameweza kutiliana saini na kampuni nyingine ya umeme wa jua ambayo itaanza kwa pemba ya mega watt 15 wapo kuangalia hatua nyinmgine za kitaalamu Zaidi .

Zanzibar tunaenda sambamba ili kuhakikisha sera ya uchumi wa bluu na kuhuisha viwanda vyetu vya ndani. Ndani ya mwaka mmoja mpaka mitatu tunatarajia kuwa na nishati mbadala ya umeme wa jua.

Akiongezea mafanikio ya shirika la umeme zanzibar (zeco) Meneja Biashara wa shirika hilo ndugu Thabit Salum Khamis. Anasema shirika la umeme zanzibar limefanikiwa kuwapitia umeme wateja 269,045 ambapo Kati ya hao kwa upande wa Unguja ni 216,784 na kwa Pemba ni 52,261 . Pia watumiaji wa mita za TUKUZA, Shirika limefanikiwa kuwaungia wateja wote wa majumbani pamoja na wateja wenye biashara ndogo ndogo ambapo jumla ya wateja 268,059 wameshafungiwa mita za TUKUZA, Unguja ni 216,059 na Pemba ni 52,067 Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2023. Aidha, shirika linatarajia kuwafungia wateja wapya wa luku wapatao 46,000 katika mwaka wa fedha 2022/2024 ambapo kwa upande wa Unguja ni 38,500 na Pemba ni 7,500. Kadhalika, katika juhudi za kupunguza upotevu wa umeme, Shirika limeshawafungia wateja wenye matumizi makubwa hoteli na viwanda Mita 112 zinazojisoma wenyewe ziitwazo Automatic Meter Reading ambazo zimeunganishwa na mfumo wa mawasiliano ambapo msimamizi anaweza kukagua mwenendo wa matumizi ya wateja hao wakati akiwa ofisini.

Lengo la mwaka huu wa fedha ni kuwafungia mita 130 wateja wakubwa ili kuendelea na juhudi za kupunguza upotevu wa umeme pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato

Kuhusu changamoto za shirika kwanza ni Upotevu wa umeme unaosababishwa kwa kiasi kikubwa na wateja wasiokua waaminifu ambao wanaiba umeme na kutumia kinyume na utaratibu

piaWananchi wasio waaminifu kuiba na kugaribu miuondombinu ya kusafirishia umeme ikiwemo kuharibu transformer na kuiba nyaya za umeme hasa za madini ya copper na kusababisha hasara kubwa kwa shirika na kuwakosesha huduma ya umeme Wananchi mbali mbali

kwa kuongezea Baadhi ya wateja kutolipa matumizi yao ya umeme kwa wakati na kwa ukamilifu.

pamoja na Ujenzi holela unaofanywa na baadhi ya Wananchi na kupelekea tatizo la kutofikika kwa baadhi ya maeneo na shirika kushindwa kufanya marekebisho stahiki hasa kuondosha tatizo la umeme mdogo n.k

**"ZECO TUNANG'ARISHA MAISHA YAKO."**

## MAADHIMISHO YA MIAKA 59 YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

**59**

**MIAKA YA MUUNGANO**



Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi

Bodi ya Wakurugenzi, Menejiment na Wafanyakazi wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) wanaungana na Watanzia wote kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** na Raisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar **Dkt Hussein Ali Mwinyi** kwa kutimiza miaka 59 ya Muungano.

Shirika la Umeme Zanzibar linajivunia mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi cha miaka 59 ikiwa ni pamoja na kuimarisha na kuboresha upatikanaji wa huduma ya nishati kwa viwango vya juu Na kutatua changamoto za umeme

**"TUPO KUNG'ARISHA MAISHA YAKO"**

Kwa mawasiliano
S.L.P 235 Mtaa wa Gulioni, Zanzibar
Simu namba: +255 2452255 (Makao Makuu Unguja)
+255 2452259 (Pemba)

Huduma kwa wateja: 0772 877 879
Barua pepe: info@zeco.co.tz
Website: HYPERLINK "http://www.zeco.tz" www.zeco.tz
Facebook, Instagram,Youtube,Twitter :ZECOZanzibar

173953



Mtoto wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Balozi Ali Karume, akizungumza na Nipashe, nyumbani kwake, Maisara mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# Makamu wa Pili SMZ: Muungano ni kila kitu

• Balozi Karume afafanua urefu wa mzizi ulivyo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HAPANA shaka hesabu ya leo ni miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Wenye Muungano wao wanapaza sauti kwamba unasaidia kuimarisha ulinzi na usalama, ikiwa ni zao la kazi bora ya marais wawili, Mwalimu Julius Nyerere kutoka Tanganyika na Sheikh Abeid Amani Karume, wa Zanzibar, hata ukapatikana msamiati Tanzania.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, anautafsiri kuwa ni zao la nia thabiti ya viongozi hao waasisi wa taifa, kwa kuzingatia uhusiano wa muda mrefu wa wananchi wa pande zote mbili .

Anasema Muungano unabaki kuwa wa kipekee Afrika na duniani kote, akiwataka wananchi wadumu wakiyaenzi, kwa kuutunza na kuulinda, ikiwa ni tunu mojawapo inayoangaza maendeleo ya Watanzania wote, ukishuhudiwa kwa kupiga hatua na kuimarika, ndani ya amani na utulivu nchini.

> Kuanzishwa kituo hicho ni kwenda sambamba na malengo ya SMZ, kuelekea katika uchumi wa buluu, ambao unalinda rasilimali baharini na kuongeza utafiti wa mazao ya bahari.

**SABABU ZA KUDUMU**

Makamu wa Pili wa Rais SMZ, anasema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unadumu kwa sababu umeundwa katika msingi muhimu wa maridhiano ya wananchi yanayotokana na undugu wa damu wa pande zote mbili.

Anarudi kwenye historia kwamba, hata kabla ya Muungano wenyewe kufanyika, tayari viongozi wa pande zote mbili katika kupigania uhuru, walikuwa na uhusiano wa karibu, huku wakishiriki katika mikutano ya kudai uhuru, iliyofanyika katika nchi mbalimbali, ikiwamo Uingereza na Ghana.

Anatoa mfano wa mkutano wa kudai uhuru uliofanyika Lancaster, Uingereza, Rais wa Tanganyika Mwalimu Julius Nyerere alihudhuria mkutano huo pamoja na Rais wa chama cha ASP, Sheikh Abeid Amani Karume, pia viongozi wengine wa vyama vya wapigania uhuru Afrika, akiwamo shujaa Kwame Nkrumah wa Ghana.

''Mara baada ya Tanganyika kupata uhuru wake Desemba 1961, watu hawakushangaa kuona Zanzibar nayo inajikomboa kutoka kwa watawala wa Kiarabu, kwa sababu viongozi wa pande mbili walikuwa wakishirikiana katika hatua mbalimbali, ikiwamo mawazo, mbinu na fikra,' anasimuilia Abdullah.

Hapo Makamu wa Rais, anajivunia mafanikio hayo ya Muungano kufaidika na matunda ya kushirikishwa katika mengi ya msingi yenye unasaba wa pande mbili, Bara na Visiwani.

**SMZ YARIDHISHWA**

Makamu wa Pili wa Rais, anasema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), inatambua mchango mkubwa wa taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar, zinavyofanya kazi kubwa kuhamasisha ukuaji teknolojia na kazi za utafiti, zinazoleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo.

Abdullah anazungumza kwa kielelezo, kwamba kuanzishwa Kituo cha Utafiti wa Bahari katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), kwa kiasi kikubwa kutasaidia kazi za utafiti katika eneo la bahari, ikiwamo kulinda rasilimali za baharini na viumbe vyake.

Anasema, kuanzishwa kituo hicho ni kwenda sambamba na malengo ya SMZ, kuelekea katika uchumi wa buluu, ambao unalinda rasilimali baharini na kuongeza utafiti wa mazao ya bahari.

Abdullah anaipongeza Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya COSTECH ya Jamhuri ya Muungano, kwa kutumia vigezo vyake, hatimaye kuiteua SUZA kufanya kazi za utafiti wa kituo cha bahari.

''Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunaridhishwa na utendaji wa taasisi za Muungano ziliopo nchini katika kuleta mageuzi makubwa ya teknolojia na ubunifu wa kazi za utafiti,' 'anasema Makamu wa Pili wa Rais, huku akitaja mifano ya taasisi hizo za Muungano, ni Benki Kuu ya Tanzania (BOT).

Hapo anafafanua majukumu makuu ya BoT, inatoa sarafu ya Tanzania, pamoja na kusimamia uchumi, pia kudhibiti taasisi za fedha ikiwamo benki zilizopo nchini.

Gavana wa Benki Kuu, Emmanuel Tutuba, hivi karibu alifika Zanzibar na kuonana na viongozi wa ngazi za juu wa SMZ, akiwamo Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi na Waziri wa Fedha ya SMZ.

Akizungumza nao, Gavana Tutuba akaahidi kufanya kazi zake kwa karibu na SMZ, ikiweka mazingira rafiki na taasisi za fedha, benki ziweke matawi yake Zanzibar, hatua itakayosaidia kuboresha mzunguko wa kuchumi, BOT ikitoa ushauri wa kitaalamu katika uchumi.

"Naahidi kufanya kazi kwa uadilifu katika pande zote za Jamhuri ya Muungano, nikiamini kwamba Zanzibar ni sehemu ya Benki Kuu, ambayo ni taasisi ya muungano katika kukuza uchumi na maendeleo,' 'anasema Gavana Tutuba.

**BALOZI ALI KARUME**

Balozi Ali Karume, mtoto wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, anasema Muungano uliopo umeleta faida kubwa kwa wananchi wa Zanzibar, ikiwamo fursa ya matumizi ya ardhi, soko la pamoja la Muungano la watu milioni 60, wakati Zanzibar ina watu milioni mbili ambapo hiyo ni fursa kubwa kwa uchumi wa Zanzibar.

Anasema, Zanzibar ina eneo ndogo la ardhi na kuwa wakati Zanzibar ilipewa eneo kubwa la ardhi la Makurunge, katika zama za uongozi wa Raisa wa Pili wa SMZ, Aboud Jumbe, ardhi hiyo alikabidhiwa na Rais wa Muungano Nyerere.

Karume, aliyewahi kuwakilisha nchi akiwa ubalozi nchini Italia, anasema Muungano umesadia kuimarisha ulinzi na usalama na kuwataka wananchi kuendelea kulinda misingi wa Muungano, ulioasisiwa na Mwalimu Nyerere, pia Mzee Karume.

Anataja kauni ya kuugana mataifa mawili, ni lazima kuna upande ukubali kupoteza mamlaka na ndicho kilichotokea mwaka 1964 kwa Tanganyika na Zanzibar.

"Zanzibar isingeweza kubakia salama kama isingeingia katika Muungano, kwa sababu kulikuwa na makundi mawili yanayovutana, wanaounga mkono utawala wa kikoloni chini ya Sultan, jambo ambalo lingesababisha misukosuko na kupoteza utulivu wa nchi," anasema.

Balozi Karume, anaungana na hoja za wataguilizi wake, kwamba ni Muungano uliosaidia kuimarisha ulinzi na usalama, hivyo anawaasa wananchi kuendelea kulinda misingi wa Muungano.

# Wasomi & wanasiasa katika butwaa la kasi, miaka miwili zimeondoshwa 15

INATOKA UK. 12

bar Kujiunga na Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organisation - IMO).

Anaendelea kwa kauli "nyingine ni ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Ushiriki wa SMZ katika masuala mbalimbali ya kimataifa na kikanda na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia."

Kwa mujibu wa Abbas, pia inajumuisha utaratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ile ya SMZ, katika kushughulikia masuala ya Muungano na uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar, katika soko la Tanzania Bara.

**TIBA YA KERO**

Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), mwanasheria Dk. Hellen Kijo-Bisimba anakiri jitihada zinazofanywa na Rais Dk. Samia kumaliza kero za Muungano zina sura ya mafanikio katika kuzitibu.

"Tunaona juhudi mbalimbali za Rais za kutaka kumaliza kero za Muungano. hasa kukutana na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa kujali mustakabali wa Taifa," anasema Dk. Hellen.

Anaongeza kuwa Rais Dk. Samia, ameshazungumzia suala la mchakato wa katiba mpya na kwamba hiyo ni muhimu kwa kila jambo, likiwamo suala la Muungano, ambalio umekuwa likilalamikiwa.

"Kwanza mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar kwa sasa yanapishana na ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tazania, hivyo suala la kuwapo katiba mpya ni la muhimu, kwani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mbili zilizoungana, lakini katiba iliyopo haiongelei vizuri kuhusu Muungano wa nchi hizo mbili," anasema.



Mwalimu Julius K. Nyerere na Shekhe Abeid Amani Karume wakipungia wananchi wakati wa sherehe za Muungano zilizofanyika Dar es Salaam tarehe 26 Aprili, 1964.

Mwanasiasa James Mbatia, ambaye alishakuwa Mwenyekiti wa chama NCCR -Mageuzi, pia yumo katika orodha ya wanaharakati waliokuwamo katika wadai wa vyama vingi vya siasa mwanzoni mwa miaka ya 1990, anausema Muungano ni muhimu, hasa katika uhalisia watu wote duniani wanaleta nguvu pamoja, akitoa mfano nchi za Ulaya, zinaendelea kuungana kwa kasi zikijua 'umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.'

Anasema Watanzania nao wamekuwa wakishuhudia jinsi ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akijitahidi kuulinda, kwa kutatua kero zake kama ambavyo imekuwa ikielezwa na wasaidizi wake.

"Ingawa sijui kero zinazotajwa kutatuliwa ni zipi, lakini inaonyesha kuwa zimepungua kutoka 25 hadi kufikia tatu, lengo likiwa ni kutaka kudumisha Muungano wetu," anasema Mbatia.

Hata hivyo, ana ushauri kwamba, ni vyema kwa Watanzania wakijiuliza kuhusu hizo kero kwamba ni zinanafasi gani, akifafanua Muungano uliozaa Tanzania unategemea ni kiongozi gani yupo madarakani na kwamba, pamoja na juhudi zinazofanywa na Rais Dk, Samia, bado kuna a haja ya kuwa na Muungano unaodumu milele, kwa kuunganisha watu wenyewe kwa utashi wa kisiasa.

Ana mtazamo wake kwamba iwapo wananchi watapewa nafasi kuelezea muungano wanaoutaka kupitia katiba mpya, manung'uniko yatapungua.


ZFDA ISO (9001:2015) CERTIFIED

SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
WAKALA WA CHAKULA DAWA NA VIPODOZI

MAADHIMISHO YA MIAKA 59 YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

59 MIAKA YA MUUNGANO



Uongozi na Wafanyakazi wa WAKALA WA CHAKULA DAWA NA VIPODOZI ZANZIBAR( ZFDA) Ofisi ya wakala wa chakula Dawa na Vipodozi wanaungana na Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dkt . Samia Suluhu Hassan na Raisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kuadhimisha miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

"KWA PAMOJA TUNALINDA AFYA YA JAMII"

OFISI YA UNGUJA
Tomondo Road, Mombasa Area,
P.o.box 3595, Zanzibar,
Tel +255242233959,
Fax 255 242233959,
Website www.zfda.go.tz,
Email info@zfda.go.tz

OFISI YA PEMBA
Kilimandege,Wete Pemba
TEL; 255242454050
Website www.zfda.go.tz
Email; info@ zfda.go.tz



Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi 173945 Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

# Rais Samia na Dk. Mwinyi wanavyofanana, penye historia, hadi kuendesha majukumu

• Wameanza siasa mwaka mmoja, kuvuka bahari, hadi urais

**Na Mwandishi Wetu**


Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi. **PICHA: MAKTABA**

NI kawaida katika siasa zote duniani nyendo zake hufanana kulingana na mtakwa ya kipindi chake, ikiwamo kiuchumi. Kuna wakati Rais wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi alishalitamka hilo kwa msemo 'kila zama na azma zake.'

Yanapoangaliwa baadhi ya mambo ya viongozi wakuu wa pande mbili za Muungano, kwa maana kati ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan wa Jamhuri ya Muungano na Dk. Hussein Mwinyi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), kuna mengi ya kihistoria, matendo hata hata kisiasa wanashabihiana.

Wakati kiumri, Dk. Samia yuko juu kwa miaka zaidi ya mitano, upande wa taaluma zao kuanzia mizizi yao inashabihiana kwa maisha, hata kitaaluma wote ni wasomi ngazi ya shahada ya uzamili, hata nyendo zao kihistoria kutumikia taaluma.

Mathalan Dk. Mwinyi alianza kutumikia taaluma yake ya udaktari wa binadamu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam, pia akafundisha katika Chuo Kikuu cha Hubert Kairuki, ndivyo ilivyo historia ya Rais Dk. Samia katika fani tofauti, lakini katika kipindi anachomtangulia Dk. Mwinyi wa SMZ.

Wote walijitosa katika siasa za ubunge kwa mara ya kwanza mwaka 2000, Dk, Mwinyi akiwa jimboni Mkuranga, Pwani na kuteuliwa kwa nafasi ya Naibu Waziri, kisha awamu iliyofuata, 2005- 2019 akawa waziri, tena katika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mambo ya Muungano (2006 - 2008). Baada ya hapo, akawa Waziri wa Ulinzi.

Hapo katika historia ya ofisi ya Mambo ya Muungano, ndiko miaka mwili baadaye tangu Dk, Mwinti kutoka, Rais Dk. Samia akafika hapo na kudumu miaka sita kwa vyeo tofauti.

Mwaka 2005 Dk, Mwinyi akavuka bahari kwenda jimboni Kwahani, Unguja ambako akaendelea kugombea, hata akachaguliwa bungeni kwa jimbo la Kwahani, Zanzibar.

Ni historia kama hiyo ya siasa, pale Rais Dk. Samia, akagombea ubunge jimbo la Makunduchi, Unguja mwaka 2010, akihama kutoka Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na kuvuka bahari kwrnda kuhuudhuria vikao vyua Bunge jijini Dodoma.

Baada mafanikio hayo, Dk. Samia akachaguliwa uwaziri akiyoutumika na Dk, Mwinyi wakiwa katika baraza moja la mawaziri, historia iliyosonga hadi 2015, akachaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, akuhama kutioka bvikao vyua bunge.

Wakati Dk. Mwinyi akiendelea na uwaziri na bunge, naye miaka mitano baadaye akatoka katika Baraza la Mawaziri la Muungano, mwaka 2020, akigombea urais Zanzibar na akaupata,hapo akahamia rasmi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, akiwa mkuu wake.

Baada ya mwaka mmoja, Dk. Samia, Makamu wa Rais wa Muungano, naye akateuliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tazania, bada ya kifo cha Rais Dk. Magufuli.

### DIRA ZA UONGOZI

Kisiasa, wote mara tu baada ya kushika nafasi ya kuongoza nchi wamekuwa tena na siasa zinazoshabihiana katika mengi. Itakumbukwa tu mara baada ya Dk. Mwinyi kukabidhiwa usukuni wa kuongoza nchi, akaweka msimamo wake wa maelewano kisiasa akitumia msamiati 'si wakati wa kufukua makaburi.'

Hilo limeendana na ushuhuda wa siasa za kirafiki Zanzibar, hata msuguoano wa kisiasa kuonekana kuzimika kwa kasi umma ukimsifu Dk. Mwinyi kwa hilo, hata itakumbukwa namna maelewano yaliyoshuhudiwa kisiasa katika serikali ya maridhiano na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, marehemu Maalim Seif Shariff Hamad wa kutoka Chama cha ACT - Wazalendo.

Ni aina ya ushuhuda unaosonga katika ngazi mbalimbali kisiasa, hata penye kifo chake Maalim Seif, ikabeba sura ya msiba wa Wazanzibari wote katika mustakabali wa kina, wa upendo na maridhiano, pasipo alama utengano, hata kweli kuthibitisha 'makaburi hayajafukuliwa.'

Dk. Mwinyi sasa kajenga utamaduni wa kila Ijumaa anawatembelea viongozi na watu mbalimbali Zanzibar, akiimarisha sura ya maridhiano na upendo, mathalan hivi karibuni, akishuhudiwa kwenye vyombo vya habari alipomtembelea aliyekuwa Rais Zanzibar, Dk. Salmin Amour.

Kimsingi, kwa staili hiyo hiyo ndiyo inayoonekana katika hulka za siasa za Rais Dk. Samia, naye mara nyingi anashuhudiwa akiwatembelea viongozo mbalimbali wastaafu na walio nje ya duru za siasa hivi sasa.

Ni msingi unaoshuhudiwa baada tu ya kuchukua uongozi wa nchi, akatumia zaidi siasa za maridhiano, akianza na mazungumzo na vyama vya siasa ambavyo vilikuwa katika vilio kadhaa, ikiwamo kufungiwa kuendesha mikusanyiko na dai la katiba mpya.

Baada ya muda kukashuhudiwa kurejeshwa katika ulingo wa mkusanyiko kisiasa, jambo ambalo limeibua pongezi nyingi kwake mkuu huyo wa nchi, hata kuimarisha jina aliliopewa la 'Mama' kwa maana ya kuwa na hulka ya mzazi wa kike, naye si mchoyo wa masihara akirejeha utani, mathalan kiongozi wa Chadema Godbles Lema akimuiota 'mwanagnu Lema; huku kiiongozi huyo akidumu na jina 'Mama.'

Ni aina ya siasa sasa, ina endana na kuachiwa kwa wanasiasa waliokuwa vifungoni, vilevile waliokimbili nchi wakirejea kutoka ughaibuni, hatua iliyoweka historia mkuu wa nchi kutoka chama tawala CCM, akipongezwa kila kukicha.

Hat8ua hiyo imejengha picha hata kwa sura ya viongozi wa vyama hata vilivyokuwa hasimu, wakijumuika na kupiga picha ya pamoja kwa furaha, kubwa kuliko yote ni pale Rais Dk. Samia kuwrka historia akalikwa, mgeni rasmi katika mkutano wa Baraza la Wanawake wa Chadema (BAWACHA), hiyiba yake akishaguiliwa sana kirafiki akikaribishwa kwa kishangilio mama.

Ni aina ya maridhiano sasa yanaaza kukabirisha nchii taasisi za kiuchumi kimataifa zinazodawi kwamba 'zilisusa'.

### UCHUMI UNAOFANANA

Mara baada ya kuingia kuongoza urais wa Visiwani, eneo mojawapo ambako Dk. Mwinyi ameamua kuwekeza ni katika Uchumi wa Bluu, akiendeleza juhudi za watangulizi wake katika awamu kadhaa, binafsi akiwapatia kupaumbele cha kipekee.

Ni aina ya uchumi ambao ndio sasa unashika kasi duniani, ukijumuisha mazao kama kilimo cha mwani, samaki na utajiri

INAENDELEA UK. 17

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

SALAM ZA PONGEZI
(1964 - 2023)



Bodi ya Wakurungenzi, Menejimenti na Wafanyakazi Wote wa Tanzania Commercial Bank Plc, tunaungana na Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mh Dk Samia Suluhu Hassan** na Raisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi **Mh Dk Hussein Ali Mwinyi** pamoja na Watanzania wote katika kuadhimisha miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

*MUUNGANO DAIMA!*

#NaKazilendelee

Makao Makuu, PSSSF Millenium Towers 2 , Barabara ya Bagamoyo, S.L.P 9300, Dar es salaam Tanzania

Simu: +255 765 767 683, +255 788 767 683, +255 658 767 683 +255 773 767 683

Baruapepe: info@tcbbank.co.tz, callcentre@tcbbank.co.tz
Baruapepe:www.tcbbank.co.tz
@tanzaniacommercial bank

217393502

# Rais Samia na Dk. Mwinyi wanavyofanana, penye historia, hadi kuendesha majukumu

INATOKA UK. 16

wote unaopatikana baharini. Hicho hicho ndicho kinashuhudiwa katika staili ya juhudi za ukuzaji uchumi kutoka kwa Rais Dk. Samia, upande wa bara, mfano hai kikitawala katika fukwe za Kilwa mkoani Lindi.

Kimsingi, zao lilitambulishwa visiwani Zanzibar miaka 30 iliyopita. Mafanikio ya uzalishaji wake yalipatikana haraka sana na kuipaisha Zanzibar, hata ikawa mzalishaji mkuu wa zao hilo duniani, ikifuatiwa na Ufilipino.

Kutokana na kwamba kilimo hicho cha mwani kinafanyika katika fukwe ya bahari, wakulima wake hawahitaji kuwa na hati miliki ya ardhi, hivyo kukifanya kuwa na nafasi kubwa, licha ya mabadiliko tabianchi yakileta changamoto.

Matumizi ya mwani inajumuisha kuwa, chakula katika nchi za Mashariki ya mbali kama barani Asia, vilevile zinatengeneza kiungo kwenye chakula kuchukua sura ya marashi na hata sabuni.



Kilimo cha Mwani, katika visiwa vya Songosongo mkoani Lindi, ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji uchumi wa bluu, upande wa Bara.

**WANAWAJIBIKA PAMOJA**

Hivi sasa, kuna Tume ya Maboresho ya Mifumo ya Taasisi za Haki Jinai Tanzania, inayohudumia jukumu la kimuungano, baada ya mzunguko mrefu katika maeneo ya bara, kukutana na taasisi na wadau mbalimbali kitaifa Tanzania Bara, hivi karibuni imepiga kambi visiwani.

Wiki mbili zilizopita chombo hicho kilipokutana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Mwinyi, ambaye akampongeza Rais wa Tanzania, Dk Samia, kuunda tume hiyo ili kuleta tija kiutendaji kwa mifumo ya hiyo kwa mahitaji ya sasa.

Dk. Mwinyi katika mazungumzo yake na tume hiyo, inayoongozwa na wenyekiti Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Othman Chande, akaeleza matarajio yake makubwa ni mapendekezo hayo yatawasilishwa kwa Rais Dk, Samia na kuonyesha marekebisho yanayohitajika katika mfumo mzima wa kimuundo wa taasisi za haki jinai, ili kuletwa ufanisi mkubwa wa utekelezaji katika kutoa kwa serikali zote mbili.

Mwenyekiti Jaji Mkuu Mstaafu Chande, anakaahidi tume hiyo itazungumza na wadau mbalimbali akitaka mifano ya asasi za kiraia na kiserikali , taasisi zinazoshughulikia haki jinai, kama vile Polisi, Chuo cha Mafunzo, Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Zanzibar, Idara ya Uhamiaji na Mahakama, kwa Unguja na Pemba.

Tume hii iliteuliwa na kuzinduliwa na Rais Dk Samia mnamo Januari 30, 2023 kutathmini na kuangalia maboresho ya mifumo ya haki Jinai Tanzania.

Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji amesema Rais Samia Suluhu Hassan na Dk Hussein Mwinyi wanapaswa kukumbuka umuhimu wa Katiba Mpya kwa kuwa Tanzania inahitaji mchakato huo uanze hivi sasa.

Wakuu hao wawili staili yao ya kazi haipishani au kuiwa mbali, hata wanaposhughylika na watui wengineo, mfano kuna wakati mwanasiasa maarufu wa Zanzibar, hivi sasa kiongizio wa chama ACT Wazalendo, Juma Duni Haji, maarufu Babu Duni akakutana na viongozi hao wakuu wa Tanzania na Zanzibar, kwa nyakati tofauti kati mwisho wa Aprili an mwanzo Mei, meaka jana akiwasilishia ujumbe wa dai la kutaka katikba mpya.

Ni mazingira ambayo hayashangazi sasa, kukiwapo dhana ya kuwapo hatua za mojea kwea moja za kiutawala zinazohusu siasa za Muungano, au zile zinazohusu utatuzi wa kero zake kwa wakati, mfano hai ni jana tu Bungeni, Waziri wa Sheria na Katiba, akatangaza sasa suala la kushugulikia hitaji la katiba mpya, mchakato unaanza wakati wowote.



# Butiku awavaa mafisadi, wezi wa kura

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, amesema watu wanaoendekeza wizi katika mambo ya uchumi na wizi wa kura, hawana maadili na si wazalendo.

Butiku amesema siku hizi kumekuwa na tabia ya watu kutokuwa wazalendo kwa kubaguana na kunyang'anyana mali na mambo ya uchumi pamoja na kuiba kura.

Akizungumza jana kwenye kongamano la kuadhimisha miaka 59 ya Muungano lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Butiku alisema wengine wanaofanya hivyo ni wale wanaojiita wasomi maprofesa na wenye shahada za uzamivu (PhD)

"Siku hizi kumekuwa na tabia ya watu kubaguana, wengine wakisema mimi nimesoma sana sasa wewe ukisoma unaacha kuwa mtu siyo kwamba umejielimisha zaidi ili uwasaidie wengine.

"Sehemu ya maadili ya wasomi ni kutumia elimu kuhudumia wale ambao hawakuipata ili wanyanyuke wawe kama wewe. Siku hizi tunanyang'anyana kwa mfano ardhi, siku hizi uchumi umekuwa wa wizi na nini ulikubaliana uongozi tunapataje tuchague kwa haki, usawa... siku hizi tunaiba kura, tunakuwa kama wahuni tu tunababaisha.

"Tena wanaobabaisha wengine ndio hao wa PHD wengine maprofesa, wengine ni wazee kama mimi hovyo kabisa huo si uzalendo, huo ni wa raia wahuni eee. Na nyie vijana msikubali wala msijifunze kuwa raia wahuni, mnaokataa taratibu zenu za utu," alisema.

Butiku alisema maadili ya Mtanzania awaye yote ni kuwa mzalendo kwa kusaidiana na kushirikiana.

Pia alisema maadili na uzalendo ni kuelewa historia yako ulikotoka, uliko na uendako na kutii, maadili na uzalendo huo.

"Katika maisha yetu ya kila siku tangu ndani ya nyumba yenu, mnavyosaidiana na kushirikiana hayo ndio maadili bila kuiga mambo mabaya wala yale ambayo huyaelewi maana kufanya hivyo utakuwa mjinga. Msijifunze kuwa raia wahuni, mnaokataa taratibu zenu za utu.

"Taifa letu kama tulivyoachiwa na waasisi wetu ni la kushirikiana, lenye utu na la kutokubaguana, na walituwekea utaratibu wa Katiba unaotuongoza namna ya kuishi," alisema.

"Wazee wetu (Amani Abeid) Karume na Mwalimu (Julius) Nyerere, walionyesha tangu awali kwamba ni wazalendo hata kabla ya uhuru wa Mapinduzi ya Zanzibar. Waliungana pamoja kuona mambo gani wanaweza kufanya ili watu wao wawe na umoja na uhuru wao katika nchi zao, walisaidiana sana," alisema Butiku.

"Tuone fursa tulizonazo ambazo zimezagaa Tanzania Bara na Zanzibar, tuzitumie kwenye maendeleo yetu, kila mtu aangalie fursa gani inamfaa kati ya zile zilizopo na wazitumie na zitawasaidia."

Naye mwanadiplomasia na mwanasiasa mkongwe, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema mpaka sasa hakuna kero za Muungano kwa sababu ziko fursa ambazo kila Mtanzania akijifunza na kugundua namna ya kuzitumia katika muungano huo ni lazima atafaidika na kuendelea kuupenda.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

Miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar 26 Aprili, 2023

"Umoja na Mshikamano Ndiyo Nguzo ya Kukuza Uchumi Wetu"



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Watanzania wote katika kumbukizi ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

173950


## Watanzania 200 waliokuwa Sudan waanza kuondolewa

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imewarejesha watanzania 200 miongoni wakiwamo wamo wanafunzi na maofisa wa ubalozi wa Tanzania waliokuwa nchini Sudan.

Hatua hiyo imekuja baada ya kuibuka kwa mapigano nchini humo yaliyoanza tangu Aprili 15, mwaka huu, yakihusisha Jeshi la Ulinzi la Sudan na Kikosi cha usaidizi wa haraka cha wanamgambo wa RSF.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, alisema Tanzania imetumia fursa ya kusimamishwa mapigano hayo kwa siku tatu iliyoanza Aprili 21, ili kuwarejesha watu wake walioko nchini humo.

Waziri huyo alisema kutokana na machafuko kuwapo katika viwanja vya ndege, walilazimika kuwapakia Watanzania hao kwenye mabasi na kuwapitisha katika mpaka wa Ethiopia. Alisema watasafirishwa mpaka Addis Ababa nchini Ethiopia ambako watachukuliwa na ndege ya Shirika la Ndege la Air Tanzania kuja nchini.

"Zilitolewa siku tatu za kusimamisha mapigano zilizoanza Aprili 21 hadi Aprili 23, mwaka huu, na tumetumia fursa hii kuwarejesha Watanzania walioko huko .Niwahakikishie kwamba, Watanzania ambao walikuja kwa ajili ya kutaka kusaidiwa na serikali, wako salama.

"Tulianza kuwasafirisha tangu jana (juzi) na hivi sasa wamefika katika mpaka wa Ethiopia. Kazi ni ngumu kwa sababu yale ni mapigano, tungeweza kutumia ndege kuwarejesha kwa pamoja, lakini haikuwezekana kwa sababu viwanja vya ndege nchini Sudani vilikuwa kwenye mapigano makali,"

"Kwa hiyo njia tuliyotumia kuwatoa kule ni ya mabasi kupitia Ethiopia na wakitoka pale watakwenda hadi Addis Ababa na pale ndipo watachukuliwa na ndege ya Air Tanzania ambayo iko tayari na siku ya kuwarejesha tutawatangazia kwa ajili ya kuwapokea," alisema. Alisema Tanzania ndio nchi ambayo imefanikiwa kuchukua raia wake wengi kutoka nchini humo.

"Namshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa ujasiri wake wa kusimamia kazi hii ya kuwarejesha Watanzania nyumbani. Hii si kazi rahisi hata kidogo, nchi nyingi ziko pale lakini ni chache ambazo zimefanikiwa kuchukua raia wake na Tanzania ndio tumechukuwa wengi kuliko nchi nyingine, wengine wamechukua 50, 20 lakini sisi tumefanikiwa kuchukua 200," alisema.

Pia alisema Tanzania imesaidia nchi nyingine kuwarejesha raia wake ikiwamo wa Uganda, Kenya, Zimbabwe, Burundi Ethiopia na Msumbiji.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

Nyumba Mpya ya vyumba 3 vya kulala sasa inauzwa.Nyumba iko Gongo La Mboto,Viwege karibu na kwa Mpemba.Nyumba inahitaji umaliziaji mdogo.

Bei:Tsh. 50 millioni lakini mazungumzo yapo.

Kwa maelezo zaidi Piga:0743800457/0686176365

---

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 119 OF 2023**
**In the Matter of the Estate of the Late LILIAN SEBASTIAN RWECHUNGURA**
**And**
**In the Matter of Petitioner for letters administrating by ALICE SEBASTIAN RWECHUNGURA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the Petitioner.

Objections to the grant should filed on or before the 16 day of 05, 2023

**Dated at DAR ES SALAAM this 25 day of 04, 2023**

Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLAN LOHAY HOLM**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba: T460 APR, CHASSIS NAMBA: 6873318 na ENGINE NAMBA: 6873318. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/143216/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**(TAARIFA YA KUSIKILIZWA SHAURI)**
**MAHAKAMA YA WILAYA SINGIDA**
**SHAURI LA RUFAA / MADAI**
**Na. 01 MWAKA 2023**
**MBUKE KWILASA.............MWOMBA RUFAA/ MAOMBI**
**VERSUS**
**NDAMO KASHINJE................MJIBU RUFAA/MAOMBI**
**WITO KWA: NDAMO KASHINJE**

Fahamu kwamba tarehe 02/05/2023 saa 8:00 ndiyo siku ya kusikilizwa shauri la Rufaa / Maombi husika.

Fahamu kwamba ikiwa hautahudhuria kama unavyoamuriwa kupitia wito huu bila sababu ya msingi, utashitakiwa kwa kosa la kudharau au kupuuza amri halali ya Mahakama.

Hati hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya MAHAKAMA hii leo tarehe 24/04/2023.

HAKIMU
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
P.O. Box 2
SINGIDA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CONSESA MALLEY HOLM**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T598 AHK .** Kwa yeyote atakaeion atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/143056/2023**

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
**AT KISUTU**
**CIVIL CASE No. 03 of 2023**
**CANARA BANK (TANZANIA) LTD**
**PLAINTIFF**
**Versus**

1. **BRIBOS COMPANY LIMITED**
2. **VUHUNGU NGAJILO ..........DEFENDANT**
3. **SALOME DICKSON SAMEJI**

**NOTICE OF DATE OF JUDGEMENT**

**TAKE NOTICE** that, the above mentioned case has been fixed for judgment on the 27 day of April 2023 at 1:00 pm

**YOU** are required to appear in this court without fail and must produce on that day all documents upon which you intend to relay in support of your case.

**GIVEN** under my hand and the SEAL of the court this 20 day of April 2023

PRINCIPAL/SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KISUTU – D'SALAAM

---

## NOTISI/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**LEGENDS AUCTION MART & GENERAL BROKERS** kwa mamlaka tuliyopewa na **VICTORIA FINANCE PLC, AKIBA COMMERCIAL BANK PLC , BRAC** na **NMB BANK** kwa mujibu wa sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,tunatoa notisi ya kulipa madeni kwenye taasisi zote nne kwa mdaiwa hapo chini ndani ya siku 7 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa marudio wa hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| s/No. | Jina la Mdaiwa | Jina la mdhamini | Dhamana | Mahali ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ROSEMARY ALOYCE MOSHA | ROSEMARY ALOYCE MOSHA | Nyumba | KIMARA TEMBONI MTAA WA MJIMPYA-UBUNGO | 03/05/2023 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea(MARUDIO). |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 au malipo kamili siku ya mnada.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0788411524/0714939933.

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**BERTHA SEKO MWASEBA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4193/0016 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **HARRISON UWATA GIRLS HIGH SCHOOL** mwaka 2015. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0867/0739 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **PANDA HILL SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **MBE/MBE/RB/308761/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDUL RAMADHANI MUSHI**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye jina la umiliki HALMASHAURI YA MSALALA yenye USAJILI NAMBA: **SM4943** na CHASSIS NAMBA: **AHTFK22G703018295.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chocote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/142309/2023**

---


## KUPOTELEWA KWA CHETI



**PRISCA S. MWAKINYONGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S. 3885-0533** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia WENDA HIGH SCHOOL mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/12603/2023**

---


## KUPOTEA KWA CHETI



**NDUGU HERBERT JUMA KASHILILAH** anatangaza kupotelewa na passport yake yenye No. **TAE148684** iliyotelewa 23rd, July,2019 na kuisha muda wake July 2029 . Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi: Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/142617**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**OSCAR H. MWANG'ONDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0471/0081** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MBOZI SCONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MBE/KYE/RB/136892/2023**

---


***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***


---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WITNESS EVERIN LEMA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye usajili namba: **T 650 BZW,** CHASSIS NAMBA: **SCP103241036** na ENGINE NAMBA: **4FE6787.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/107584/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**
**KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 16/2022**
***(Asilia shauri la Rufaa Jinai Na. 01/2022 kutoka Mahakama ya Wilaya ya Momba, na pia Asilia Shauri la Jinai Na. 380/2021, Mahakama ya Mwanzo Tunduma.)***
**LIPITE MAHENGE..............................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**SISTA ROBENY........................ MJIBU RUFAA NA. 1**
**PRISCA YUSUFU........................MJIBU RUFAA NA. 2**

**KWA BWANA:**
1. **SISTA ROBENY**
2. **PRISCA YUSUFU**

**POPOTE MLIPO – TANZANIA**

Mnaamriwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya tarehe **15/05/2023** siku ya Jumatatu saa **3:30 asubuhi** bila kukosa.

**ELEWENI KWAMBA** mkikosa kufika siku hiyo, shauri litasikilizwa upande mmoja bila ninyi kuwepo na uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 03/04/2023.

HAKIMU
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
P.O. Box 2
SINGIDA

---


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***



**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# AZAM YAINOLEA MAKALI SIMBA SC

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Kalimangonga Ongala ameanza mikakati ya kuimarisha safu ya ushambuliaji kuelekea nusu fainali ya kombe la Shirikisho Tanzania, FA, dhidi ya Simba.

Safu ya ushambuliaji ya Azam inaongozwa na Prince Dube na Idrissa Mbombo na sasa wamepewa jukumu la kuhakikisha wanaiondoa Simba katika michuano hiyo.

Pia safu ya ulinzi nayo inanolewa ili kuwa makini zaidi kwa sababu wameona ubora wa Simba katika safu ya ushambuliaji ambayo ni hatari na wako makini wanapopata nafasi.

Azam watakuwa wenyeji wa Simba katika nusu fainali hiyo Mei 5 mwaka huu katika dimba la Nangwanda Sijaona, Mtwara.

Akizungumza na Nipashe jana, Ongala alisema amekuwa akiwafuatilia Simba katika mechi wanazocheza na kuona ubora wao hasa safu ya ushambuliaji na hivyo wanaendelea kujipanga.

Alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu uwanja wanaokwenda kuutumia wote watakuwa ugenini hali hiyo haitakuwa na kisingizio endapo mmoja wapo atapoteza .

"Hatuhitaji sababu kwa kuwa Nangwanda Sijaona wote ni wageni, uwanja, kikubwa tunaendelea kujiimarisha na kufanyia kazi kikosi chetu ikiwemo safu ya ushambuliaji na ulinzi kwa kuangalia ubora wa wapinzani wetu," alisema Kalimangonga.

Aliongeza kuwa kitendo cha kumuanzisha Mbombo katika mechi mbili mfululizo huku Dube akitokea benchi ni kwa ajili ya mipango yao na sio sababu ya kumpumzisha (Prince) kwa ajili ya Simba.

"Sio kweli Dube amepumzishwa kwa ajili ya mechi ya Simba au tunamuandaa Mbombo bali tunafanya mabadiliko ya safu ya ushambuliaji kulingana na wapinzani tunaokwenda kukutana nao, kwa mechi ya Simba tunaenda kujiandaa vizuri," alisema.

Aliongeza: "Tunahitaji kupambana kutafuta matokeo katika mchezo wetu huo wa nusu fainali, na naamini mechi itakuwa ngumu kwa sababu Simba tuliwafunga katika ligi na hawatakubali kupoteza kwa mara nyingi hasa ukizingatia huu mchezo akifungwa mmoja anaondolewa kwenye mashindano," alisema Kalimangonga.

Alisema wanahitaji kupambana katika matokeo hayo ili kubadilisha mwenendo mzuri kwa Azam kwa msimu huu baada ya kushindwa kufikia malengo yao katika Ligi Kuu Tanzania Bara.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule za Sekondari za jijini Dar es Salaam wakicheza mpira wa magongo katika viwanja vya Jakaya Kikwete jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

## *Video ya kwanza bendi ya CHAMUDATA hewani*

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya muziki wa dansi ya wanawake iliyopo chini ya umiliki wa Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (CHAMUDATA), imetupia video ya wimbo wa vita ya ukatili kijinsia katika mitandao ya kijamii.

Mwenyekiti wa wanawake CHAMUDATA, Deborah Nyangi, aliutaja wimbo huo kuwa ni 'Tanzania Bila Ukatili Wa Kijinsia Inawezekana' na kuuongeza kuwa video yake ilirushwa hewani tangu wiki iliyopita.

"Kwa sasa ukiingia kwenye mitandao ya kijamii utakutana na video ya wimbo huo ambao ni maalum kwa kuhamasisha vita dhidi ya vitendo vya ukatili ndani ya jamii nchini,"alisema Deborah.

Alisema wanawake na watoto ndio ambao hukumbwa na ukatili wa kijinsia, na kwamba wameamua kutunga wimbo huo, ili kusaidia jamii kuepuka ukatili huo ili kila kundi liwe salama.

Deboraha alisema hali ni mbaya kuanzia majumbani, shuleni hadi mitaani, na kuongeza kuwa vitendo vya ukatili vya ukatili wa kijinsia vimekuwa ni sehemu ya maisha kwenye baadhi ya jamii.

"Kupitia wimbo wetu, ninaamini tutakuwa na mchango mkubwa wa kuelimisha umma wa Watanzania katika kumbi za burudani tunakopiga muziki na hata kwingineko kwani watakasikiliza ujumbe wa wimbo huu na kuufanyia kazi, watakuwa ni mabalozi wetu,"aliseam.

Deborah alisema bendi hiyo inaundwa na wanamuziki 15, huku akiwataja baadhi yao kuwa ni Anna Mwaole, yeye mwenyewe (Deborah), Luiza Mbutu, Khadija Kimobitelna Anneth Kushaba.

Aliwataja wengine kuwa ni Tabu Mambosasa (wimbaji), Getrude Joseph (kinanda), Sarah Sauti (mwimbaji), Bright (drums) na Taji Mbaraka anayeungurumisha gita la besi, lakini pia ana uwezo wa kupiga magita yote na kuimba.

## Minziro akerwa na wachezaji, kukaa nao chini

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Geita Gold limesema limesikitishwa kupoteza mchezo wao dhidi ya Tanzania Prison kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kukubali kichapo cha mabao 3-1 nyumbani kwao.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Geita Gold, Fred Minziro alisema wachezaji wake walicheza tofauti na maelekezo aliyowapa kabla ya mchezo huo.

"Wachezaji wangu wameshindwa kufuata maelekezo niliyowapa kitendo ambacho kimeigharimu timu yangu nikiwa nyumbani," alisema Minziro.

Alisema makosa aliyoyaona atayafanyia kazi mapema ili yasijitokeze kwenye michezo iliyobakia ya Ligi Kuu kwa msimu huu.

"Nitakaa na wachezaji wangu na kuwaelekeza pale walipokosea na kuanza kujipanga upya kwa ajili ya michezo iliyobakia, kwani malengo ni kuendelea kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao," alisema Kocha huyo.

Aliwataka mashabiki wasikatishwe tamaa na matokeo waliyoyapata na badala yake waendelee kuwapa ushirikiano ili waweze kumaliza michezo yao salama.

## Rais wa riadha kuzikwa leo Arusha

**Na Shufaa Lyimo**

MWILI wa aliyewahi kuwa Rais wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Francis John unatarajiwa kuzikwa leo Jumatano nyumbani kwake mkoani Arusha.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana asubuhi kutoka mkoani humo Katibu wa Chama cha Riadha Arusha, Rogath John alisema mazishi hayo yatafanyika majira ya saa kumi jioni.

"Kesho (leo) tunatarajia kuupumzisha mwili wa ndugu yetu Francis nyumbani kwake maeneo ya Moshono Boma Siara hapa Arusha," alisema John.

Alisema leo saa nne asubuhi mwili utapelekwa kanisani kwa ajili ya ibada na baadae kwenda kupumzishwa kwenye nyumba yake ya milele.

Alisema anashukuru wamepata ushirikiano mkubwa tangu msiba huo ulipotokea kutoka kwa viongozi mbalimbali wa serikali pamoja na wadau wa mchezo wa riadha.

John alifariki duniani April 22 mwaka huu kwenye hospitali ya KCMC Moshi mkoani Kilimanjaro, ikiwa kifo chake kimetokana na ajali ya gari iliyotokea maeneo ya maji ya Chai nje ya mji wa Arusha akitokea jijini Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### KANE AZIDI KUWINDWA

KLABU ya Manchester United inaimarisha juhudi zao za kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane msimu huu wa joto, huku nahodha huyo wa England mwenye umri wa miaka 29 akitarajiwa kutosaini mkataba mpya na klabu yake ya utotoni. (***Telegraph***)

### ZAHA MKATABA MNONO

MSHAMBULIAJI wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried amepewa mkataba mpya wenye utakaomfanya kulipwa pauni 200,000 kwa wiki. Mkataba wa sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na anazivutia Arsenal, Chelsea na Paris St-Germain. (***Guardian***)

### BEI YA ONANA

AC Milan imeweka bei ya pauni milioni 35 kwa mlinda mlango wa Cameroon, Andre Onana, huku Chelsea ikiripotiwa kumnyatia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. (***Goal***)

### AUBAMEYANG KUREJEA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Pierre-Emerick Aubameyang mwewnye umri wa miaka 33 ndiye anayelengwa zaidi na Barcelona kurejea Nou Camp msimu huu wa joto ili kumsaidia mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski. (***Sky Sports***)

### FIRMINO AJIPELEKA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 31 ana nia ya kujiunga na Barcelona mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu - lakini klabu hiyo ya Hispania haina nia ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. (***Marca***)

### ALLISTER ANYATIWA

KIUNGO wa kati wa Brighton, Alexis Mac Allister mwenye umri wa miaka 24, ataondoka pale Seagulls msimu huu wa joto, lakini anapanga kubakia kwenye Ligi ya England. Liverpool inaongoza mbio za kuwania mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Argentina, lakini Tottenham Hotspur, Chelsea na Newcastle United pia zimeonesha nia ya kutaka kumsajili. (***90Min***)

### GAVI HAONDOKI

KIUNGO wa kati wa Hispania, Gavi mwenye umri wa miaka 18 ameihakikishia klabu ya Barcelona kuwa hana mpango wa kuondoka Nou Camp msimu huu wa joto, licha ya kuwa bado hajakubali mkataba mpya na anafuatiliwa na klabu kadhaa barani Ulaya, ikiwemo Chelsea. (***Sport***)

### MIN-JAE AGOMBEWA

KLABU ya Manchester City itachuana na Manchester United, Liverpool na Tottenham Hotspur kumsajili beki wa Korea Kusini, Kim Minjae mwenye umri wa miaka 26 kutoka Napoli kwa pauni milioni 40. (***Sun***)

### LAPORTE ANAITAKA BARCA

MLINZI wa Hispania, Aymeric Laporte mwenye umri wa miaka 28 hana furaha Manchester City baada ya kushindwa kupata nafasi ya kuanza mara kwa mara na anataka kujiunga na Barcelona. (***Relevo***)

### RAPHINHA ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imepanga kumrejesha winga wa zamani wa Leeds United anayeichezea Barcelona, Raphinha kwenye Ligi Kuu ya England. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 27 anaweza kuunganishwa pale St James' Park na mlinzi wa Uturuki, Arda Guler mwenye umri wa miaka 18, na kiungo mwenzake, Ferdi Kadioglu mwenye miaka 23 kutoka Fenerbahce. (***Mirror***)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HUKUMU YA UBINGWA EPL

**Ni Man City vs Arsenal leo, mechi itakayotoa mwelekeo anayeweza kuwa bingwa Ligi Kuu England...**

**MANCHESTER,** England

MECHI ya Jumatano hii kati ya Manchester City na Arsenal inatarajiwa kuwa ya kusisimua zaidi, huku mshindi akiwa na nafasi nzuri kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England.

**Man City wanaingia kwenye mchezo huo wakiwa nafasi ya pili kwenye msimamo na pointi tano nyuma ya Wa shikabunduki hao, lakini mabingwa hao watetezi wana michezo miwili mkononi na hawajafungwa katika mechi 16 katika michuano yote.**

Arsenal, kwa upande wake, hawajaonja kichapo katika mechi 12 - mara ya mwisho kupoteza walipokuwa wenyeji wa City - lakini wamekwama wiki za hivi karibuni kufuatia sare tatu mfululizo.

Majeraha sio tatizo kwa wenyeji City chini ya kocha Pep Guardiola kwani ana takriban kikosi fiti kabisa cha kuchagua.

Beki Nathan Ake alikosa katika ushindi wa nusu fainali Jumamosi wa Kombe la FA dhidi ya Sheffield United kutokana na tatizo la misuli ya paja na anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa mara nyingine.

William Saliba amekaa nje katika mechi tano zilizopita za Arsenal akiwa na tatizo la mgongo na haionekani kama atakuwa tayari kurejea kwa ajili ya mechi hii ya kiporo.

Takehiro Tomiyasu na Mohamed Elneny hawakuwepo kwa muda mrefu na hawatacheza tena msimu huu.

**TAKWIMU**

Man City wameshinda mechi zote sita za ligi ya nyumbani dhidi ya Arsenal chini ya Guardiola kwa jumla ya mabao 17-3, mara ya mwisho kufungwa wakiwa nyumbani na Washikabunduki ilikuwa Januari 2015.

Arsenal wamepoteza mechi 11 zilizopita za ligi kuu dhidi ya City, ukiwa ni msururu wao mrefu zaidi wa kupoteza dhidi ya wapinzani wao katika historia ya ligi, huku wakiwa wameruhusu angalau mara mbili katika mechi sita kati ya 11 zilizopita za ligi.

Erling Haaland ameifungia City mabao 32 ya ligi, mabao mengi zaidi kuwahi kufungwa na mchezaji katika msimu kwa michezo 38 katika mashindano hayo huku 20 akifunga kwenye dimba la Etihad.

Bukayo Saka amefunga mabao mawili ya mwisho ya Arsenal kwenye ligi dhidi ya City, ingawa yote mawili aliyapata kwenye mechi za nyumbani. Mchezaji wa mwisho wa Arsenal kufunga nyumbani na ugenini dhidi ya City katika msimu alikuwa Theo Walcott msimu wa 2016-17.

City wana uzoefu mkubwa kuelekea mwishoni mwa msimu na wameifanya Etihad kuwa ngome katika wiki za hivi karibuni - wakishinda mechi 11 mfululizo katika mashindano yote.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI


MANCHESTER CITY
VERSUS
ARSENAL

1 | 1.56
X | 4.06
2 | 4.91

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# KOVACIC AZIGONGANISHA MAN CITY, BAYERN

**LONDON,** England

MATEO Kovacic anahisi yupo "nyumbani" pale Chelsea huku kukiwa na ripoti kwamba, raia huyo wa Croatia analengwa na Manchester City na Bayern Munich.

Kovacic anakaribia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na Chelsea, na kushindwa kwake kuweka bayana kuhusu mkataba mpya kumesababisha mapendekezo ya kutaka kuondoka.

City wanaweza kuwa sokoni kwa ajili ya kuongezewa safu ya kiungo katika dirisha lijalo la usajili, huku nahodha wa klabu hiyo, Ilkay Gundogan akidaiwa kutathmini ofa ya mkataba kutoka kwa Barcelona.

Kovacic pia amekuwa akihusishwa kuungana tena na kocha wa zamani wa Chelsea, Thomas Tuchel, ambaye amepata mwanzo mgumu wa maisha kule Bayern tangu kuchukua nafasi ya Julian Nagelsmann mwezi uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amekuwa chini ya makocha watatu tofauti wakati wa msimu wa misukosuko pale Stamford Bridge, na bado anaridhika kuendelea kukaa hapo Magharibi mwa London.

Akizungumza na vyombo vya habari vya klabu, Kovacic alisema: "Nimekuwa hapa kwa miaka mitano tayari, muda unakwenda, na nimekuwa Chelsea kwa muda mrefu zaidi ya klabu zangu zote.

"Ninahisi kweli, niko nyumbani. Hakuna kitu cha kutopenda London. Familia yangu inafurahia, ambayo hunirahisishia. Chakula ni sawa, labda si kama Italia au Hispania! Lakini London ni ya kushangaza.

"Naweza tu kusema mambo mazuri kuhusu London na England. Tunajisikia vizuri sana hapa."

Kovacic ameanza mechi tatu kati ya nne za Chelsea tangu Frank Lampard arejee katika klabu hiyo kama kocha wa muda mapema mwezi huu, ikijumuisha mikondo yote miwili ya kushindwa kwa jumla ya 4-0 dhidi ya klabu yake ya zamani ya Real Madrid katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# *Ten Hag amtarajia Varane fainali FA*

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag anatarajia Raphael Varane kurejea katika utimamu wa mwili kwa wakati ili kushiriki katika mechi ya fainali ya Kombe la FA kati ya Manchester United dhidi ya wapinzani wao wa jiji, Manchester City.

Varane alitolewa wakati wa mapumziko baada ya kupata jeraha la kifundo cha mguu wakati wa mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Sevilla, ambayo Mashetani Wekundu walipoteza kwa jumla ya mabao 5-2.


Beki mshirika wa kati wa Varane, Lisandro Martinez, alijeruhiwa kwenye mguu na hivyo hatakuwepo kwenye mchezo huo.

Huku nahodha wa klabu hiyo Harry Maguire akiwa amesimamishwa, Luke Shaw alishirikiana na Victor Lindelof katikati ya safu ya ulinzi huku United ikifika fainali ya 21 ya Kombe la FA iliyoweka rekodi sawa na kwa ushindi wa mikwaju ya penalti Jumapili dhidi ya Brighton na Hove Albion.

United sasa itamenyana na wapinzani wao City wanaowinda kutwaa kwa mara ya mara tatu taji hilo katika fainali itakayopigwa Uwanja wa Wembley Juni 3, na Mashetani Wekundu wana matumaini ya kuwa na Varane.

Alipoulizwa kama Varane anaweza kushiriki fainali ya pili ya kombe la nyumbani la United msimu huu, Ten Hag aliiambia talkSPORT: "Nafikiri hivyo, ndio. Varane kwa fainali ya kombe hilo anaweza kurejea."

Varane ameichezea United jumla ya mechi 27.



CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# SHIME AITA 46 KWA MCHUJO TIMU ZA TAIFA WANAWAKE

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa timu ya taifa ya Wanawake, Bakari Shime amewaita wachezaji 46 kutoka timu mbalimbali za wanawake kwa ajili ya mchujo wa kusaka watakaoingizwa kwenye vikosi vya timu ya taifa.

Taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Soka Mpira wa Miguu Tanzania, (TFF), chini ya Afisa Habari na Mawasiliano, Cliford Ndimbo ni kwamba wachezaji wao wameteuliwa kutoka timu za Ligi Daraja la Kwanza, La pili na Mabingwa wa Mikoa.

Wachezaji wote walioitwa wanatarajia kuingia kambini Mei Mosi na baada ya hapo watachujwa kupata watakaokwenda kwenye timu ya wakubwa, Twiga Stars, chini ya miaka 20 na 17.

Wachezaji hao wamechaguliwa baada ya kuonekana kufanya vizuri wakiwa na timu zao zinazopambana kwenye ligi hizo.

Walioteuliwa kuingia kambini ni Diva Godfrey wa Mapinduzi Queens), Mariam Shaaban, Melkia William, Kulwa Rocket, Sarah Lucas, Ester Maseke, Semeni Juma, Jamila Celestine, Hellen Steven, wote wa Bunda Queens.

Wengine ni Naomi Samuel, Restuta Innocent, Sabina Alex, Saada Mabele, Mariam Salum, Allie Sebastian, Mary Elia, Safafina Thadei wa Geita Gold Queens, Glory Ibrahim na Winfrida John, na Edna Madamba wa Oysterbay Queens, Happnines Daffa wa Masala Queens, Eva Elikana na Maria Jusel wa Mabibo Queens.

Wengine walioitwa ni Mwanaidi Maulid, Yusta Zonobia, Frida Abdallah, Lidya Maximilian wote wa TSC Queens, Kulwa Nkwabi wa Ukerewe Queens, Angel Wilbert na Petronila Simon wa Lengo Queens, Zuhura Hamsini na Hidah Suleiman wa Mbagala Queens, Mage Ageth wa Sayari Queens.

Shime wamewaita pia Mikaela Daffa, Furaha Kifaru, Hellen Hamisi, Saidath Yohana, Nusra Leonard, Jesca Bernard,Amina Musa, wote kutoka Bilo Queens, Saada Ayoub wa JMK Park Queens, Marry Joseph, Adrofina Simon na Rukia Hussein kutoka Ruangwa Queens, Sundi Ramadhani yeye anakipiga na timu ya Kinondoni Queens.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kariakoo jijini Dar es Salaam wakicheza mpira wa Kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nabi: Hatujabweteka

INATOKA UK 24

Aidha Kaze alisema licha ya mwanzo mzuri ugenini bado wana dakika 90 kwenye uwanja wa Mkapa katika mchezo wao wa marudiano.

"Ninaomba wachezaji wasibweteke na ushindi tulioupata ugenini wafahamu bado tuna dakika 90 ambazo zinatusubiri kwenye uwanja wetu wa nyumbani," alisema.

Kocha huyo alisema wataandika historia endapo watamaliza hizo dakika kwa ushindi na kuomba mashabiki wajitokeze kwa wingi siku ya mchezo wa lengo la kuwapa nguvu wachezaji.

"Tutaandika historia ya kuitoa Rivers United kama tutafanikiwa kuingia hatua ya nusu fainali kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika,".

Kikosi cha Yanga kimerejea nchini jana na kuingia kambini moja kwa moja kwa ajili ya mchezo huo wa Jumapili kwa ajili ya kutafuta ushindi ambao utawapeleka katika hatua ya nusu fainali.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 26/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5374 | Gwangju vs Jeju Utd | 2.34 | 3.03 | 2.83 |
| 13:00 | 5728 | Gangwon vs FC Seoul | 2.94 | 2.99 | 2.30 |
| 13:30 | 2581 | Suwon City vs Daegu | 2.45 | 3.23 | 2.55 |
| 13:30 | 3027 | Jeonbuk Hyundai vs Daejeon Citizen | 1.90 | 3.40 | 3.45 |
| 14:35 | 2589 | Shanghai Shenhua vs Changchun Yatai | 1.91 | 3.24 | 3.60 |
| 14:35 | 3126 | Shenzhen vs Tianjin Teda | 3.54 | 3.39 | 1.88 |
| 15:00 | 1400 | Arba Minch Kenema vs Saint George FC | 5.60 | 4.05 | 1.48 |
| 15:30 | 5142 | Shukura vs Dinamo Batumi | 7.28 | 4.47 | 1.35 |
| 16:00 | 1319 | Terengganu vs Pahang FA | 1.71 | 3.49 | 4.21 |
| 16:00 | 2536 | Bkma Yerevan vs Van Yerevan | 3.38 | 3.01 | 2.12 |
| 16:00 | 2565 | FC Gyori Eto vs Budafoki Mte | 1.96 | 3.14 | 3.55 |
| 16:00 | 3127 | NK Osijek vs Istra | 1.83 | 3.18 | 4.00 |
| 17:00 | 1657 | FK Sloga Simin Han vs NK Posusje | 1.71 | 3.42 | 4.46 |
| 17:00 | 3804 | Shkendija vs Sileks | 1.41 | 3.70 | 6.20 |
| 17:00 | 5707 | FC Telavi vs FC Samtredia | 2.37 | 3.11 | 2.80 |
| 18:00 | 1483 | Fasil Kenema vs Hawassa Kenema SC | 1.86 | 3.05 | 4.24 |
| 18:00 | 1747 | Volos vs Panathinaikos | 10.40 | 4.99 | 1.28 |
| 18:00 | 2874 | AEL Limassol vs Olympiakos Nicosia | 1.69 | 3.36 | 4.76 |
| 18:00 | 4066 | Kraluv Dvur vs Motorlet Prague | 2.54 | 3.29 | 2.43 |
| 18:05 | 5910 | Dinamo Zagreb vs Vsnk Varazdin | 1.26 | 4.92 | 8.81 |
| 18:30 | 4998 | Zlin vs Bohemians | 2.80 | 3.28 | 2.39 |
| 18:30 | 5772 | Zbrojovka Brno vs Ceske Budejovice | 2.02 | 3.53 | 3.32 |
| 19:00 | 2124 | Aris Salonica vs Olympiakos | 4.20 | 3.24 | 1.89 |
| 19:00 | 2774 | Nordsjalland vs Copenhagen | 2.69 | 3.36 | 2.33 |
| 19:00 | 2873 | Omonia Nicosia vs Pafos FC | 2.50 | 2.99 | 2.73 |
| 19:00 | 3663 | Stabaek vs Brann | 3.93 | 3.52 | 1.78 |
| 19:00 | 4323 | Talaea El Gaish vs Ghazl EL Mahallah | 1.99 | 3.02 | 3.97 |
| 19:00 | 4461 | Ararat Yerevan vs Alashkert Martuni | 3.98 | 3.10 | 1.90 |
| 19:00 | 4969 | Sepsi Osk vs CFR Cluj | 1.81 | 3.31 | 4.08 |
| 19:30 | 3056 | Sturm Graz vs Austria Vienna | 1.52 | 3.95 | 5.03 |
| 20:00 | 5078 | Birkirkara vs Mosta | 1.83 | 3.62 | 3.62 |
| 20:10 | 2191 | HNK Gorica vs Hajduk Split | 3.02 | 3.18 | 2.15 |
| 20:30 | 3638 | Atletico Madrid vs Mallorca | 1.40 | 4.00 | 7.99 |
| 20:30 | 3845 | Getafe vs Almeria | 1.84 | 3.25 | 4.20 |
| 20:30 | 4728 | Sparta Prague vs Viktoria Plzen | 1.64 | 4.01 | 4.54 |
| 21:00 | 5285 | AEK Athens vs PAOK | 1.74 | 3.38 | 4.86 |
| 21:15 | 4154 | Lillestrom vs Bodo Glimt | 3.11 | 3.42 | 2.06 |
| 21:30 | 2426 | Nottingham vs Brighton | 5.43 | 4.12 | 1.51 |
| 21:30 | 2459 | Servette Geneva vs FC Zurich | 2.40 | 3.25 | 2.78 |
| 21:30 | 3035 | Zamalek vs Ceramica Cleopatra | 2.09 | 3.11 | 3.51 |
| 21:30 | 5116 | Rapid Vienna vs RB Salzburg | 4.01 | 3.75 | 1.68 |
| 21:30 | 5601 | St. Gallen vs FC Lugano | 1.90 | 3.58 | 3.58 |
| 21:45 | 1579 | Chelsea vs Brentford | 1.66 | 3.70 | 4.60 |
| 21:45 | 2272 | West Ham vs Liverpool | 3.57 | 3.53 | 1.90 |
| 22:00 | 4549 | Inter vs Juventus | 2.04 | 3.27 | 3.59 |
| 22:00 | 5003 | Sheffield Utd vs West Bromwich | 2.06 | 3.19 | 3.44 |
| 22:00 | 5821 | Manchester City vs Arsenal | 1.56 | 4.06 | 4.91 |
| 22:30 | 3136 | Famalicao vs Porto | 5.81 | 4.10 | 1.46 |
| 23:00 | 1389 | Celta Vigo vs Elche | 1.30 | 4.82 | 8.63 |
| 23:00 | 5945 | Rayo Vallecano vs Barcelona | 4.32 | 3.40 | 1.77 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipashe Jumatano Aprili 26, 2023




Hukumu ya ubingwa EPL

UKURASA 21

# Simba kimbinu zaidi Morocco

## ●●● Kocha Robertinho asema wamejiandaa kwa ushindi tu, watapigania heshima, rekodi...



Wachezaji wa Simba wakiwa Dubai wakisubiri kuunganisha ndege kuelekea nchini Morocco. **PICHA: SIMBA**

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Simba, Robertinho Oliviera amesema amejiandaa kimbinu zaidi, kuelekea mchezo wa marudiano wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca.

**Simba tayari imewasili salama nchini Morocco tayari kwa ajili ya mchezo huo dhidi ya wenyeji wao hao itashuka dimba ni Ijumaa ya Aprili 28 mwaka huu kwenye uwanja wa Mohammed V, nchini humo katika mji wa Casablanca.**

Akizungumza na Nipashe, Robertinho alisema kuwa maandalizi waliyoyafanya kuelekea mchezo huo wa marudiano ni mazuri na hawatakuwa wanyonge kwa sababu malengo yao ni kutaka ushindi.

Alisema ana imani kubwa na wachezaji wake kuonyesha kiwango kizuri zaidi walichokionyesha kwenye mechi ya kwanza waliyocheza uwanja wa Benjamin Mkapa na kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

"Tunajua mechi dhidi ya Wydad Casablanca itakuwa ngumu sana, lakini tumejiandaa na mipango yetu ni kufikia malengo tuliyojiwekea kama timu," alisema.

"Sisi sio timu nyepesi tena watu watuheshimu tunaweza kwenda ugenini na tukafanya kitu, tunawaheshimu Wydad, lakini hatutacheza kinyonge pale Casablanca tumekuja kupigania heshima ya klabu hii kubwa," aliongeza Robertinho.

Alisema wanatambua umuhimu na ugumu wa mechi hiyo na wanacheza kwa pamoja na kuwa makini na safu ya ushambuliaji ya Wydad Casablanca, mechi iliyopita walitengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia.

Robertinho alisema wamewaona Wydad Casablanca wanapocheza nyumbani na kutakiwa kuwachunga sana kila sehemu ndani ya uwanja ili kurejea nchini wakiwa tayari wametinga nusu fainali.

Alisema anachokiangalia zaidi ni kuhakikisha wanakuwa makini katika mchezo huo ambao wanahitaji kutafuta matokeo mazuri ili kuwapeleka kucheza nusu fainali ikiwa ni mipango yao kwa sasa.

## Nabi: Hatujabweteka

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema ushindi walioupata ugenini dhidi ya Rivers United ya Nigeria haina maana wamefuzu kucheza nusu fainali ya kombe la Shirikisho Afrika.

Amesema wanadakika 90 zingine zilizosalia ambazo ni muhimu kwao kuzitumia vizuri nyumbani na wachezaji wanatakiwa kusahau matokeo yaliyopita na kuangalia mechi ijayo.

Yanga inatarajia kushuka dimbani Jumapili hii wakiwa wenyeji wakiwakaribisha River United katika dimba la Benjamin Mkapa Dar es Salaam, baada ya kufanikiwa kurejea na ushindi wa mabao 2-0 kutoka nchini Nigeria.

Akizungumza na Nipashe jana, Nabi alisema kushinda ugenini haina sababu ya wako kuwa tayari wamefanikiwa kwa asilimia kubwa kufuzu nusu fainali kwa sababu bado wana kibarua cha dakika 90 za kipindi cha pili.

Alisema kila mchezaji anatambua namna walivyopoteza dhidi ya timu hiyo mwaka 2021 na sababu wanazitambua na wamezifanyia kazi, wachezaji hawatakiwi kuridhika na matokeo waliyoyapata Nigeria.

"Tunatambua wapinzani wetu Rivers United sio timu mbaya na rekodi ya kupoteza mbele yao mwaka 2021 tunakumbuka, mechi zote tutapambana kupata ushindi wa jumla ili kusonga mbele kwenye hatua hii ya kimataifa.

Kushinda mechi ya ugenini ni mafanikio, lakini hatujaridhika kuishia hapo lazima tupambane kushinda mechi ya nyumbani na lazima wachezaji waonyeshe juhudi ili kupata matokeo mazuri," alisema Nabi.

Naye Kocha msaidizi, Cedric Kaze alisema nyota wao, Bernard Morrison ni majeruhi na hakuwepo katika mchezo uliopita dhidi ya Rivers United baada ya kuumia kwenye mazoezi.

Alisema Morrison alikuwa katika mipango ya mchezo uliopita na Rivers United, lakini hakufanikiwa kucheza baada ya kupata shida ya misuli na mazoezini.

"Hatukuweza kulazimisha kucheza mechi iliyopita na kumuacha apone na tunatarajia kuwepo kwenye mipango ya mechi ijayo kwa sababu ni mchezaji muhimu na anaweza kufikia katika eneo la hatari na kutengeneza madhara kwa wapinzani na kupata matokeo chanya," alisema Kaze.

Alisema watamtumia kwenye mchezo wa marudiano kwani ni mchezaji mwenye uzoefu wa kutosha kwani ameshacheza michezo kama hiyo.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >